# Nipashe


Jumamosi Aprili 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581288

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT TZS.1,104,580,144 KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU! SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Mwalimu** twisheni asakwa kwa madai kulawiti mwanafunzi

UKURASA 5

# Wabunge wabebeshwa zigo madudu ripoti ya CAG

UKURASA 2



George Mlawa Fatma Karume



Baadhi ya Waumini wa dini ya Kiislamu madhehebu ya Answar Sunni, wakishiriki swala ya Eid El Fitri katika uwanja wa Mtekelezo, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

UKURASA WA 3

## MSAMAHA BIL. 22/- WATOLEWA RIBA KODI ARDHI

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amesema Sh. bilioni 21.9 ambazo ni riba ya malimbikizo ya kodi ya ardhi zimesamehewa kutokana na msamaha uliotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan...

## Bei za mchele, nyama zapaa kuelekea Eid el Fitri

UKURASA 3

## RC, Askofu wakoleza moto mapambano dhidi ya ushoga

UK. 9 & 15


MICHEZO YANGA SC: SAFARI HII HATUWAACHI NG'O UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Rais wa Zanzibar Alhaj Dk.Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Mufti Mkuu wa Zanzibar Shekhe, Saleh Omar Kaabi pamoja na viongozi wengine, baada ya kuwasili katika Masjid Mushawal Mwembeshauri, jijini Zanzibar jana, kuhudhuria ibada ya swala ya Ijumaa. **PICHA: IKULU.**

# Wabunge wabebeshwa zigo madudu ripoti CAG

**Na Christina Mwakangale**

KATIBU wa Bunge Mstaafu, George Mlawa, amesema wabunge ndio wanaopaswa kubeba lawama ya kile kilichojiri kwenye ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mwaka 2021/22 kwa kuwa hawajawajibika ipasavyo katika maeneo yao ya uwakilishi.

Amesema ziko kasoro zilizobainika kwenye ripoti ikiwamo ubadhirifu wa fedha na rushwa katika taasisi hususani kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya umma.

Mlawa aliyasema hayo juzi, jijini Dar es Salaam, baada ya kutoa maoni yake mbele ya Tume ya Kuangalia namna ya Kuboresha Mifumo ya Hakijinai, inayoongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Othman Chande.

Alisema miongoni mwa mambo aliyowasilisha kwa tume hiyo ni eneo la kisiasa ambako ndiko chanzo cha utawala bora.

"Wabunge ndio wawakilishi wa wananchi. Kwa mujibu wa Ibara ya 8 ya Katiba ndiyo msingi, wanatumia nguvu ya uwakilishi, wamewatuma. Huwezi kuwa na utawala bora palipo na rushwa," alisema Mlawa ambaye aliwahi kuwa kwenye nafasi hiyo kwa takriban miaka tisa.

"Mfano kwenye suala la ununuzi wa ndege, Rais alishangaa imeongezeka takribani mara tatu kutoka dola milioni 37 hadi milioni 86. Kuna Kamati za Bunge zinafika 18 za aina mbalimbali kwani hayo hawayaoni hadi CAG apite kukagua? Kuna takribani wawakilishi 395, Rais atafanya mambo mangapi?" alihoji.

Mlawa alitaja maoni mengine aliyotoa ni kuhusu taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ikikabidhiwa kwa Rais, ijadiliwe bungeni ili waliobainika kukiuka haki na utawala bora wahojiwe na Bunge.

"Ijadiliwe bungeni kwa sababu ndiko kunakobainika kinachoendelea kwenye jamii, lakini sasa hiyo tume haina nguvu hata bajeti yake ni kiduchu," alisema Mlawa.

**FATMA KARUME**

Wakili wa Kujitegemea, Fatma Karume ambaye naye alifika mbele ya tume hiyo kuhojiwa alisema, miongoni mwa mambo sita aliyowasilisha ni kuwapo kwa mahakama maalumu ambazo zitashughulikia mashauri ya jinai, ili kuongeza kasi ya usikilizwaji.

"Nimezumgumza na tume mambo sita, hasa kuhusu upatikanaji wa kuwa na mahakama ya kudumu ya kesi za jinai na sasa kesi zinafanyika Mahakama Kuu.

"Kuwe na usajili wa kesi za jinai kwenye mahakama za mwanzo. Ila ninashauri kuwapo mgawanyo wa kesi za jinai na madai ili kuongeza usikilizwaji kwa haraka," alisema Fatma.

Pia alisema mahakama ipewe bajeti ili kuandaa mazingira hayo ya utendaji kazi na kuwapo ubobezi au mahakimu waliojikita eneo moja la uamuzi, katika mashauri kuhusu jinai au madai.

Maoni mengine alisema ni kuwapo sheria ya dhamana ili kutoa haki hiyo kwa wote wenye vigezo vya kudhaminiwa na si masharti kuwabana wengine.

"Tuache unyanyapaa, mtu ambaye anahitajika kutoa dhamana vigezo viwe wazi si kwamba, awe mwajiriwa au nini. Tuna mikataba ya kimataifa ya kulinda haki, tuheshimu katiba yetu.

"Watu wanaopaswa kutoa dhamana wasinyanyapaliwe kwamba lazima awe mtumishi wa umma, yaani mimi siwezi kumpa mtu, ndugu dhamana sababu si mtumishi?" alihoji.

Kadhalika, alisema ametaka kuwapo miongozo ya namna ya kutoa uamuzi, kwa kuwa hivi sasa hakimu hutoa hukumu ya kesi kulingana na ridhaa yake na baadhi yake zikitofautiana miongoni mwa watoa uamuzi, licha ya aina ya makosa kufanana.

"Mahakama ziwe na specialization (ubobezi) kwa sababu kuna level (hatua) za mahakimu kwa sababu hakimu aliyetoka chuoni juzi atatoaje hukumu ya miaka 10. Hana uzoefu kwa sababu anakuwa hajui maisha na unampa uwezo mtu atoe hukumu ya miaka 30.

"Kuna baadhi ya uamuzi una utu ndani yake. Mhitimu kijana atakavyotoa hukumu anaweza kuhukumu, ili kujipa umaarufu, lakini mzoefu unaangalia athari itakuwaje? Wawepo mahakimu wa kuendesha kesi za madai na jinai ili kuongeza uwanja wa utoaji haki na hili linawezakana," alisema huku akisisitiza kuwa ili kupuka rushwa lazima kuwapo na miongozo.

"Mfano mtu kaua kwa kutumia panga, mwingine aliua ila kwa kutumia nguvu zake mwenyewe, au mwingine alitumia silaha nzito, hapa ukiwa na uzoefu aina ya uamuzi utapishana kulingana na mazingira ya tukio.

"Kuwapo aina ya hukumu, iwe kali kulingana na matendo yake. Haki jinai zimekuwa haziaminiki. Kilichopo ni hakimu kupanga hukumu kwa ridhaa yake," alisema Wakili Fatma.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
07 - 10 - 2022

TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kutaarifu umma kuwa siku ya Jumatatu tarehe **10-10-2022** kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM PORT** kuelekea **MBAGALA**, gari hizo zenye namba za usajili:

**T 203 DYJ / T 837 DJB**
**T 204 DYJ / T 887 DJB**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 25.00 Upana - mita 5.00 Kimo - mita 4.70**

3. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza

NANGE AUCTIONMART AND DEBT COLLECTORS LTD
P.O. Box 16284-ARUSHA (HQ), TEL. 0754 748323
MANYARA BRANCH
Dealers in: AUCTIONEERS, DEBT COLLECTORS COURTBROKERS, PROPERTY VALUERS AND COMMISSION AGENTS

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KWA WADAIWA WA SACCOS ZA NANJARA REHA, MAKIIDI NA , KENI MENGENI

Kwa idhini tuliyopewa na Nanjara Reha Saccos, Keni Mengeni saccos na Shimbi saccos tutauza kwa mnada wa hadhara mali zilizoorodheshwa hapa chini ambazo ziliwekwa dhamana wakati wa kuchukua mkopo.

| S/N | JINA | DHAMANA | MAHALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ATANSIA KANJE | SHAMBA | ROMBO | 5 MAY 2023 Nakuendelea Saa 4 asubuhi |
| 2 | PETER SWAY | KIWANJA | ROMBO | 7 MAY 2023 Nakuendelea saa 5 asubuhi |
| 3 | RICHARD SHIRIMA | SHAMBA | ROMBO | 5 MAY 2023 Nakuendelea saa 8 mchana |
| 4 | NOVATI ASSEY | SHAMBA | ROMBO | 7 MAY 2023 Nakuendelea saa 3 asubuhi |
| 5 | DONATILA TARIMO | SHAMBA | ROMBO | 7 MAY 2023 Nakuendelea saa 4 asubuhi |
| 6 | REGINA NGOMA | SHAMBA | ROMBO | 7 MAY 2023 Nakuendelea saa 8 asubuhi |
| 7 | PRISCUS TARIMO | SHAMBA | ROMBO | 5 MAY 2023 Nakuendelea saa 3 asubuhi |
| 8 | LEYA WOISO | SHAMBA | ROMBO | 9 MAY 2023 Nakuendelea saa 3 asubuhi |
| 9 | JEROME JOHN | SHAMBA | ROMBO | 9 MAY 2023 Nakuendelea saa 3 asubuhi |
| 10 | BARNABA DAMIAN | SHAMBA | ROMBO | 9 MAY 2023 Nakuendelea saa 3 asubuhi |
| 11 | DENIS NGAREKU | SHAMBA | ROMBO | 7 MAY 2023 Nakuendelea saa 6 mchana |

**MASHART YA MNADA**
1: Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei iliyofikiwa katika mnada, salio litalipwa ndani ya siku 14 toka tarehe yam nada huo
2: Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mnada wa siku 14 atakuwa amepoteza haki yake mnada utarudiwa na 25% aliyolipa haitarudishwa
3: Wateja wataruhusiwa kukagua mali husika kabla ya mnada

Mawasiliano: 0766538295

## HABARI KITAIFA




Wachuuzi wa mahindi ya kuchoma wakifanya biashara katika eneo la hifadhi ya barabara ya Bagamoyo, eneo la Mbezi Shule, Dar es Salaam juzi, licha kuwepo tangazo la zuio lililowekwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). **PICHA: SABATO KASIKA.**

# Msamaha wa bilioni 22/- watolewa riba kodi ardhi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, amesema Sh. bilioni 21.9 ambazo ni riba ya malimbikizo ya kodi ya ardhi zimesamehewa kutokana na msamaha uliotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Aidha, kuanzia Julai 2022 hadi Machi, 2023 wakati wa kipindi cha msamaha huo, wamiliki 9,188 wamenufaika huku Sh. Bilioni 32 zikikusanywa ikiwa ni deni la msingi.

Hata hivyo, kutokana na baadhi ya wananchi kupata vikwazo kujua makadirio na deni la msingi na riba itakayosamehewa, Wizara imefanya maboresho katika mfumo mzima wa utunzaji kumbukumbu za ardhi, utozaji wa kodi na utoaji wa huduma za sekta ya ardhi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maboresho yaliyofanyika kwenye mifumo unaowezesha wamiliki wa ardhi kupokea ujumbe kupitia simu za mkononi, Waziri Mabula alisema katika msamaha huo baadhi ya wananchi walishindwa kunufaika ikiwamo taratibu zinazowataka kufika katika ofisi za ardhi ili kukadiria na kujua deni la msingi na riba itakayosamehewa.

"Miongoni mwa maboresha makubwa yaliyofanyika katika kipindi hiki kifupi ni kuboresha mifumo ili iweze kutuma ujumbe mfupi wa maandishi unatumwa kwa wadaiwa wote kuwakumbusha kulipa kodi kwa wakati kupitia simu za viganjani," alisema.

Alisema hadi sasa zaidi ya ujumbe 84,000 wa simu umetumwa kwa wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi zikiwa na deni la msingi la takribani Sh. bilioni 115 ambazo zinatarajiwa kukusanywa katika mikoa 25.

"Aidha, kwa mkoa uliobaki ambao ni Dar es Salaam zoezi hili linaendelea na ifikapo tarehe 30 Aprili, 2023 wamiliki wa ardhi katika mikoa yote ya Tanzania Bara watakuwa wametumiwa ujumbe kupitia simu za mkononi kuhusiana na madai ya kodi ya pango la ardhi,"alisema.

Alibainisha kuwa hatua hiyo inatarajia kuongeza mapato ya yanayotokana na sekta ya ardhi.

"Wananchi wote kuwa wakiona ujumbe katika simu ukianza na neno "ARDHI" wajue ni ujumbe sahihi na unatoka Wizara ya Ardhi ukiwakumbusha kulipa kodi kwa wakati ili wanufaike na msamaha uliotolewa na Rais Samia ambao mwisho ni Aprili 30, 2023," alisema.

Alisema wizara itachukua hatua za kisheria ikiwamo kuwafikisha mahakamani wadaiwa wa kodi ya pango la ardhi ili kufidia kodi husika au kupendekeza ubatilisho wa milki kama masharti ya umiliki yanavyojielekeza.

"Natoa wito kwa wamiliki wa ardhi wenye madeni kuchangamkia nafuu iliyotolewa na Rais ya kulipa madeni yao ya msingi ili wasamehewe riba ndani ya muda uliotolewa," alisema.

# Bei mchele, nyama zapaa kuelekea Eid

**Na Halfani Chusi**

BEI za bidhaa zimepanda maradufu sokoni kwa mchele uliokuwa ukiuzwa Sh. 3,000 kwa kilo umefikia Sh. 4,000 huku baadhi ya wafanyabiashara wakidai hawafahamu sababu za kupanda.

Uchunguzi wa Nipashe uliofanywa kwenye baadhi ya masoko Dar es Salaam, umebaini mchele wa basmati maarufu kwa kupikia biryani, umepanda kutoka Sh. 4,000 kwa kilo hadi Sh. 7,500.

Mfanyabiashara wa nafaka kwenye soko la Ilala, Juma Mnyawami, alisema kabla ya kukaribia sikukuu ya Eid el fitri ambayo kwa Tanzania inaadhimishwa leo, mchele walikuwa wanauza Sh. 3,000 kwa kilo lakini kwa sasa unauzwa Sh. 3,700 hadi Sh. 4,000.

Mfanyabiashara mwingine wa nyama eneo hilo, Bezaleli Mgongolwa, alisema kilo moja iliyokuwa ikiuzwa Sh. 8,000 imefikia Sh. 10,000.

"Nyama imepanda sana, bei yake ipo juu mpaka kwenye machinjio. Hata hivyo, tunauza kilo moja Sh 10,000 lakini haitulipi, ilitakiwa tuuze Sh. 12,000 kwa sababu bei ya manunuzi ipo juu.

"Bei ya kuku wa kisasa nayo imepanda kidogo kutoka Sh. 6,500 hadi Sh. 7,500. Kila msimu wa sikukuu unapofika bei zimekuwa zikipanda," alisema.

Mfanyabiashara wa karoti kwenye soko la Tandale, Zuhura Malekela, alisema kiroba cha bidhaa hiyo kilikuwa kikiuzwa Sh. 45,000 lakini kwa sasa kimefikia Sh. 80,000.

"Bei zimepanda sana na kufanya biashara kuwa ngumu, tunanunua vitu gharama, wateja walio wengi wanapokuja wanashindwa kununua, wanarudi nyumbani hawajanunua kitu na tunashindwa kupunguza ili kutokupata hasara," alisema.

Mfanyabiashara mwingine wa nyanya soko la Mwananyamala, Moshi Tamimu, alisema walikuwa wananunua boksi moja la nyanya kwa Sh. 50,000 lakini kwa sasa limefikia Sh. 80,000.

Mfanyabiashara wa pilipili kwenye soko la Mabibo, Riziki Salumu, alisema kiroba cha debe saba lililokuwa likiuzwa Sh. 60,000 kwa sasa kinauzwa Sh. 200,000.

"Wafanyabiashara na wateja wote tunalia hatujui hatima yake, labda serikali iingilie kati suala hili itafute chanzo cha kupanda kwa bidhaa hizi, maana sisi wenyewe hatujui sababu kama ni bei ya usafirishaji au ununuzi shambani imepanda hatufahamu lakini kwa sasa tunanunua vitu ghali,"alisema.

Maimuna Ali, aliyekutwa kwenye soko la Kariakoo akitafuta mahitaji kwa ajili ya sikukuu, alisema ameshindwa kupata mahitaji sawa na matarajio kutokana na mabadiliko ya bei na kuiomba serikali kudhibiti mfumuko wa bei hasa wakati wa msimu wa sikukuu.

"Nimekuja hapa sokoni kununua mchele nimejiandaa kwa kilo moja Sh. 3,000 nimekuta inauzwa Sh. 3,500 tena huu bado sio ule mzuri kabisa," alisema.

Heri Kitula alisema ameshangazwa na bei ya kitunguu ilivyopanda kutoka Sh. 80,000 kwa gunia mpaka Sh. 300,000.

"Hali ni ngumu sana, nimekuja kununua kitunguu, lakini nimeshindwa, gunia limepanda linauzwa zaidi ya Sh. 200,000 hii ni hatari.

"Ninaomba serikali iangalie namna ya kukabiliana na hali hii, kitunguu kimoja kinauzwa Sh. 300 hadi Sh. 500 kulingana na eneo, wenye vipato vya chini kwa sasa ndio wanapata maumivu zaidi," alisema.






Esther Klement kutoka Idara ya Masoko Vivo Energy, akipanda mti na Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Mivinjeni, Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SKONGA ya EATV kupanda miti 1,000 shule Dar, Pwani

**Na Mwandishi Wetu**

KIPINDI cha SKONGA kinachoruka kupitia Runinga ya East Africa TV kwa kushirikiana na VIVO ENERGY TANZANIA, wamefanikiwa kupanda miti 1,000 kupitia kampeni yao ya utunzaji na utoaji elimu kuhusu mazingira ambayo imepewa jina la 'PANDA MTI ISHI KIJANI'.

Mkururugenzi Mtendaji VIVO ENERGY TANZANIA, Khady Sene, akizungumzia kuhusu kampeni hiyo, alisema kwa kutambua umuhimu wa vijana, wanaamini kundi hilo ndiLo chachu ya uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira endapo litapewa elimu hiyo na kuzitambua athari za uharibifu wa mazingira.

Sene alisema waliona ni sahihi zaidi kushirikiana na East Africa TV kupitia kipindi cha SKONGA kwa kuwa kimekuwa na wafuatiliaji wengi ndani na nje ya nchi huku kundi kubwa lengwa likiwa wanafunzi.

"Lengo letu kubwa ni kujenga tabia ya mazingira kwa vijana kwa sababu kwa kufanya hivi, tunajenga kitu kikubwa ambacho kitakuwa mazoea kwenye maisha yao ya kila siku na hii ikiwaingia zaidi vijana tunaondokana na mabidiliko ya tabia nchi," alisema.

SKONGA na VIVO ERNEGY walianza rasmi kampeni hii ya kupanda miti Machi 2, mwaka huu, mpaka mwishoni wa mwezi huu. Mpaka sasa, wameshatembelea shule 10 zilizoko Dar es Salaam na Pwani na kila shule imepanda miti 100 ikiwa miti 50 ya kivuli na 50 ya matunda.

Kampuni ya VIVO ENERGY TANZANIA ambao ni wauzaji wa nishati ya mafuta wenye vituo vya ENGEN, ililenga zaidi kutoa elimu kwa vijana shuleni ili wakue wakiwa na uelewa kuhusu utunzaji wa mazingira na kujua madhara ya ukataji wa miti.

# Mkumbo acharuka serikali kuingilia ajira vyuo vikuu

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

MBUNGE wa Ubungo (CCM), Prof. Kitila Mkumbo, ameitaka serikali kurekebisha makosa kwa kile alichokiita 'urasimu wa serikali' katika kuingilia mfumo wa ajira za watumishi wa vyuo vya umma vya elimu ya juu.

Sambamba na hilo, ameshauri serikali kuviacha vyuo hivyo kujiendesha ili kulinda uhuru wa kitaaluma.

Akichangia mjadala wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/24 uliohitimishwa juzi, Kitila alisema ni vyema serikali ikarekebisha jambo hilo ili kuepusha urasimu na kujiingiza kwenye vyuo vikuu.

"Bunge lilitunga Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya 2015 (Sheria ya Vyuo Vikuu). Lengo lilikuwa kulinda uhuru wa kitaaluma katika vyuo vikuu na vyuo vikuu vimeanzisha vyombo vyao vya kujiendesha na kujitawala. Kwa hiyo, kazi kubwa ya serikali ilikuwa kutoa sera na mwelekeo na kutoa rasilimali lakini uendeshaji wa vyuo vikuu unakuwa ndani ya vyuo vikuu vyenyewe.

"Kule kuna vyombo vikuu viwili, kuna baraza la chuo kikuu, kuna seneti. Seneti ni kama wabunge, hili ni jambo la msingi sana kwa hiyo ni lazima tulielewe na lipo hivyo duniani.

"Sasa hizi nyenzo zimewekwa ili vyuo vikuu vijiendeshe, vilinde uhuru wa kitaaluma. Kwa hiyo jambo moja la msingi ambalo lazima tulirekebishe ni kuepusha urasimu wa kawaida kuiingiza kwenye vyuo vikuu. Kwa mfano, vyuo vikuu duniani na hapa Tanzania siku zote, huwa vinaajiri watumishi wake na ndiyo maana kwenye sheria yetu ambayo nimeisoma, jukumu namba 5 la mabaraza ya vyuo vikuu ni kuteua maofisa wa taasisi. Maana yake waajiri wa vyuo vikuu ni mabaraza ya vyuo vikuu; na ajira za vyuo vikuu ni za vyuo vikuu husika.

"Sasa nataka niulize mnatusaidiaje hili jambo kulirekebisha? Katika miaka ya hivi karibuni, nadhani 2015/16, tumeamua ajira za vyuo vikuu zinaendeshwa na serikali kupitia sekretarieti ya ajira," alisema.

Prof. Mkumbo alieleza kushangazwa na uhamisho wa wahadhiri wa vyuo vikuu vya umma, akisema jambo hilo ni la kipekee kwa Tanzania kwa kuwa halikpo katika vyuo vikuu vingine duniani.

"Hili jambo ni 'perculiar' kwa Tanzania. Haliko vyuo vikuu vyovyote duniani. Huwezi kuhamisha mwalimu kutoka chuo kikuu kimoja kwenda chuo kikuu kingine. Mwalimu wa Chuo Kikuu cha Oxford, akitaka kwenda Cambridge anaomba aajiriwe na Cambridge, lakini huwezi kukuta serikali inamhamisha mwalimu kutoka Cambridge kwenda Oxford. Hiyo duniani haipo.

"Kwa hiyo hili jambo ni lazima mliangalie. Mviachie vyombo ambavyo tumeundwa kisheria vyombo vya ajira. Utumishi waache vyombo vya ajira vifanye kazi zake. Kitila Mkumbo, akitaka kwenda Chuo Kikuu cha Dodoma ana anaomba, labda chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa mfano, kati ya maprofesa wachache wa mazingira na uchumi, mmemtoa pale mkaenda kumtupa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Nyerere cha Kilimo na Teknolojia, ambacho hakina wanafunzi," alisema.

**MAPROFESA 180**

Katika mchango wake, Kitila Mkumbo, alisema hivi sasa kuna maprofesa 180 hawana pensheni na kwamba wako waliostaafu wakiwa wameondoka na Sh. milioni 10 hadi 20.

"La mwisho, ni kuwaombea maprofesa walioajiriwa baada ya mwaka 1978, kabla ya PPF kuanzishwa. Hawa watu hawakuwa kwenye pensheni, waliwekwa katika mfumo wa bima.

"Kuna kitu kinaitwa SSSS, Senior Staff Supper Scheme. Hawa maprofesa, wameondoka chuo kikuu wamepewa Sh. milioni 10, milioni 20. Sasa wamebaki maprofesa 180 hawana pensheni, wapo tu. Tunaomba Mheshimiwa Simbachawene (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma), jambo hili limalizike ili tutunze heshima ya watu ambao wametumika katika nchi hii miaka 30, miaka 40 katika utumishi wa vyuo vikuu." alisema Mkumbo.

**RIDHIWANI AMJIBU**

Akijibu hoja ya Mkumbo, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Ridhiwan Kikwete, alikiri ni kweli maelezo aliyoyatoa yana ukweli.

"Nataka nikiri mbele ya hili Bunge lako Mheshimiwa Spika kwamba, maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo yana ukweli kabisa. Nini kimefanyika, nini kimefikisha hapo, serikali ilishakutana na uongozi wa vyuo vikuu vya umma, wakiongozwa na Dean (kiongozi) wao ambaye ni 'Vice Councilor' (Makamu Mkuu wa Chuo cha Ardhi. Mazungumzo yamefanyika, nimwombe Prof. Mkumbo na wenzake katika eneo la Chuo Kikuu, watupe nafasi serikali namna ya kuliangalia.

"Nini zilikuwa sababu za kutufikisha hapa tulipofika, lakini nini kifanyike ili tuweze kuondoka hapa tulipofika twende mbele kwa kasi zaidi. Nataka nikuhakikishie kwamba dhumuni la serikali kuchukua mamlaka ya vyuo vikuu na kuyafanya ya kwake, zipo kada za kiutawala lakini zipo kada za walimu, kwa maana ya wakufunzi wetu.

"Kada hizi mbili treatment zake (namna ya kuziangalia) ni tofauti ndugu Watanzania. Kada ya utawala imeendelea kubaki chini ya utumishi, lakini kada ya wale wenzetu ambao ni wakufunzi imeendelea kuratibiwa katika jicho la mbali lakini mambo yote yanaendelea ndani ya vyuo vikuu vyenyewe," alisema.

## HABARI KITAIFA

# Mahakama yabatilisha hukumu utakatishaji fedha

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani imebatilisha hukumu na kuwaondolea adhabu waliokuwa maofisa wa Benki ya CRDB Tawi la Meru, waliotiwa hatiani na kuamriwa kulipa faini jumla ya Sh. milioni 200 kwa kutakatisha Dola za Marekani 5,468,699.25.

Mahakama pia imeamuru faini yoyote iliyolipwa irejeshwe kwa waliolipa na warufani waachiwe huru mara moja.

Hukumu ya Mahakama ya Rufani ilitolewa mjini Arusha juzi mbele ya jopo la majaji watatu, Shaaban Lila, Jaji Lugano Mwandambo na Patricia Fikirini, baada ya kuikubali rufani iliyowasilishwa na Boniface Mwimbwa na Elias Ndejembe.

Warufani walitiwa hatiani na Mahakama Kuu mbele ya Jaji Issa Maige kwa kosa la kutakatisha fedha, walihukumiwa kulipa faini Sh. milioni 100 kila mmoja na wakishindwa watatumikia kifungo cha miaka mitano jela kila mmoja.

Boniface Mwimbwa na Elias Ndejembi wanadaiwa kwa tarehe tofauti kati ya Novemba, 2009 na Februari, 2011 ndani ya wilaya, manispaa na mkoa wa Arusha, walipitisha hundi 17 za Dola za Marekani 5,468,699.25 kwa kuidhinisha kufunguliwa kwa akaunti namba 02J1036325000 inayomilikiwa na Moyale Ujasiriamali wa Vito na madini ya thamani.

Pia waliidhinisha akaunti namba 0232036310500 ya Ogembo Mitchel Chacha na akaunti namba 02J2036310600 ya Gregg Motachwa Mwua katika Benki ya CRDB, Tawi la Meru.

Katika kesi hiyo upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi 10 na vielelezo 47 na washtakiwa hawakuwa na mashahidi, walijitetea wenyewe.

Mahakama iliwatia hatiani na kuwapa adhabu hiyo baada ya kuona upande wa mashtaka ulikuwa na ushahidi wa kutosha kuthibitisha mashtaka dhidi ya warufani.

Pia mahakama ilijiridhisha kwamba, warufani walitenda makosa hayo kutokana na taaluma waliyokuwa nayo kwani walikuwa mameneja katika benki hiyo.

Warufani baada ya hukumu na kutiwa hatiani, walipinga hatia na adhabu waliyopewa wakiwa na sababu 11.

Upande wa warufani uliwakilishwa na mawakili Moses Mahuna na Hellen Mahuna wakati upande wa Jamhuri uliwakilishwa na Wakili wa Serikali Mkuu, Zakaria Ndaskoi.

Miongoni mwa sababu za rufani, inadaiwa hatia kwa mrufani namba mbili, inatokana na upelelezi mbavu wa kesi na kwamba, taarifa iliyowasilishwa mahakamani ambayo washtakiwa walisomewa na kujibu mashtaka ilikuwa batili.

Upande wa Jamhuri ulidai warufani hawakunyimwa haki wakati wa usikilizwaji na kwamba, taarifa na hatia haikuwa mbaya kwa upande wao.

Jopo baada ya kupitia hoja zilizowasilishwa na pande zote lilisema kwamba, ilikuwa ni wajibu kwa upande wa mashtaka, kurekebisha taarifa kwa mujibu wa kifungu cha 276 (2) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA).

Mahakama ilisema hilo halikufanyika, kulingana na maamuzi mengi ya mahakama, na kwamba ilikuwa vibaya kuwahukumu warufani wakati kuna mapungufu ya wazi.

"Katika rufani hii, kama ilivyoelezwa hapo juu, inahusisha tofauti ya wazi kati ya maelezo na ushahidi ambao ulibakia bila kurekebishwa na marekebisho yalipaswa kufanywa kabla ya kufungwa kwa kesi kwa upande wa mashtaka," lilisema jopo.

Jopo linasema tofauti imechangiwa na upande wa mashtaka kuongeza hesabu na mahakama inakubaliana na hoja ya Wakili Mahuna, kwamba ushahidi ulikuwa na upungufu wa kuweza kuthibitisha kuwa kila mrufani alihusika katika hundi zote 15 kama inavyodaiwa na upande wa mashtaka.

Mahakama baada ya kutathmini, iliona ushahidi unaonyesha kuwa hatia ilikuwa na makosa hivyo inabatilishwa.

"Hukumu za warufani zinabatilishwa na adhabu inaondolewa, inaamriwa kwamba warufani waachiwe huru mara moja isipokuwa kama zipo sababu zingine za kuendelea kuwashikilia.



Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, akipanda mti kwa kushirikiana na madereva wa Bodaboda, katika eneo la Mtaa wa Lumumba, Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwalimu wa twisheni asakwa madai ulawiti

**Na Mohab Dominick,**
TABORA

MKUU wa Mkoa wa Tabora, Dk. Batilda Buriani, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani hapa kumsaka na kumkamata mwalimu (jina halijatajwa) kwa madai ya kumlawiti mmoja wa wanafunzi wake waliokuwa wakisoma masomo ya ziada (twisheni) kwake.

Dk. Buriani amesema mwalimu huyo anadaiwa baada ya kufanya kitendo hicho kwa mwanafunzi huyo aliyekuwa akisoma moja ya shule zilizoko Manispaa ya Tabora, amekimbia. Agizo hilo alilitoa juzi wakati akizungumza na viongozi mbalimbali wa dini na serikali mkoani hapa wakati wa hafla fupi ya kufuturisha iliyofanyika katika viwanja vya ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Alisema serikali hawezi kuendelea kuvumilia vitendo vya kikatili vinavyofanywa na baadhi ya watu wasio waadilifu.

Dk. Buriani alisema hivi karibuni akiwa kwenye shughuli za Bunge jijini Dodoma, alipokea taarifa za tukio la mwalimu huyo ambaye wazazi na walezi walimwamini na kumkabidhi watoto wa darasa la tatu na la nne ili awafundishe masomo ya ziada, Alisema wanafunzi wakienda kusoma masomo hayo, baadhi yao walikuwa wakipewa kazi na kutoka nje na kubaki na mwanafunzi huyo na kumfanyia kitendo hicho. Wazazi wa mtoto huyo, alisema waligundua kuwapo kwa tabia hiyo baada ya mwanafunzi huyo kukataa kwenda shule na walipomwadhibu ndipo akaeleza vitendo anavyofanyiwa na mwalimu huyo. "Kwa kweli tukio hili limenisikitisha sana. Mtoto alifanyiwa vipimo na kukutwa ni kweli ametendewa hivyo. Kesi iko polisi inakwenda mahakamani licha ya mwalimu huyu kukimbia. Ninaagiza atafutwe na kukamatwa haraka iwezekanavyo ili sheria ichukue mkondo wake," aliagiza.

Dk. Buriani alisema wamepanga kuendelea kukagua vituo vya kulelea watoto yatima na kupita shuleni mara kwa mara kwa kushirikisha viongozi ngazi za vijiji.

Sheikh wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Tabora, Ibrahimu Mavumbi, amewataka viongozi wa dini kuendelea kukemea ukatili wa kijinsia katika maeneo yao ya ibada na kudhibiti viashiria vya ndoa za jinsia moja kwa kuwa, jambo hilo halimpendezi Mungu.

# Waharibifu vyanzo vya maji waonywa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI imewaonya wanaoharibu vyanzo vya maji na kufanya shughuli za kibinadamu kwenye mito inayotiririsha maji kupeleka mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Morogoro kwamba hatua zitachukuliwa dhidi yao.

Wakati kauli hiyo ikitolewa baadhi ya maeneo yakiwamo ya mkoa wa Morogoro, kumekuwa na ukataji wa miti na uharibifu wa mazingira.

Katibu Tawala Msaidizi masuala ya Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Morogoro, Dk. Rozalia Rwegasira, aliyasema hayo wakati wa ugawaji wa miche ya karafuu na mazao ya viungo kwa wakulima wanaolima kandokando ya mito pamoja na vyanzo vya maji kwenye mito tegemezi iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

Dk. Rwegasira alisema hatua ya serikali ya mkoa huo kupiga marufuku inatokana na vyanzo vya maji zikiwamo chemichemi zinazopeleka maji kwenye mito, kuharibiwa kutokana na shughuli za kibinadamu zinazohusisha kilimo, kuchoma mikaa na kukata kuni.

Alisema kutokana na tishio hilo, kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF), wameanza mkakati maalumu uhifadhi wa mazingira katika vyanzo vya maji kwenye mito tegemezi inayopeleka maji kwa wakazi zaidi milioni 11 wa mikoa hiyo mitatu.

"Kutokana na athari hizo zilizoanza kujitokeza, kuna kila sababu ya kupanda miti yenye faida kama mikarafuu kwa ajili ya kutunza mazingira na kuhifadhi vyanzo vya maji ambayo pia, itawafaidisha kiuchumi wakulima na kuachana na miti isiyo na faida," alisema.

Ofisa Programu wa Maendeleo Endelevu Afrika wa WWF, Happness Minja, alisema katika kutekeleza mpango huo, wameamua kutoa bure miche 20,000 ya miti ya karafuu kwa wakulima wanaolima ili waweze kupanda na kisha kujinufaisha kiuchumi. Alisema mpango huo utahusisha maeneo ya vyanzo vya chemichemi hai zinazotiririsha maji na kujaza vijito na mito ambako kutapandwa miti rafiki ikiwamo ya matunda. Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, Chesco Lwaduka, alisema katika mkakati huo wa kutunza mazingira na vyanzo vya maji, halmashauri hiyo imefanya utafiti unaonyesha inahitaji miche 1,113,042 ya karafuu, mdalasini miche 12,155,578, pilipili manga miche 5,825,212 na iliki miche 5,452,709.

Mkuu wa Kidakio cha Ruvu kati kutoka Ofisi ya Bonde la Wami/Ruvu, Richard Mwasenga alisema upandaji wa miti hiyo utasaidia kingo za mito na mmomonyoko wa ardhi.

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Simba, Yanga robo fainali michuano CAF

**SIMBA** na Yanga zinatarajia kushuka tena dimbani wikendi hii kupeperusha bendera ya Tanzania katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Wawakilishi hao wa Tanzania wametinga hatua ya robo fainali, ikiwa ni rekodi ya kwanza kuwekwa kwa klabu za hapa nchini kutinga hatua hiyo kwa wakati mmoja.

Wekundu wa Msimbazi kama wanavyofahamika wao leo watakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuwakaribisha Wydad Casablanca katika mechi ya kwanza ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Yanga yenyewe iko ugenini Nigeria. Yanga ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya Kombe la FA, wanapambana katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na watavaana na Rivers United ya nchini humo. Timu hizo zote zitarudiana baada ya wiki moja na mshindi wa jumla ataingia hatua ya nusu fainali.

Katika kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele, kila timu inatakiwa kupambana kusaka matokeo chanya katika mechi za mkondo wa kwanza na kurahisisha kibarua pale watakaporudiana, iwe nyumbani au ugenini.

Simba na Yanga zimeshafanya makubwa katika mashindano mbalimbali wanayoshiriki, zimefanya usajili mzuri, zimecheza mechi mbalimbali za kimataifa na kwa kifupi wachezaji wake wameshapata uzoefu wa kupambana kwenye michuano hiyo ya CAF.

Wawakilishi hao wa Tanzania wanatakiwa kuongeza umakini na tahadhari katika mechi zote mbili watakazocheza ili kujiweka kwenye nafasi ya kupata ushindi, wachezaji kuongeza utulivu kutasaidia kutawala mchezo.

Wakati Simba inatamba imejipanga kurejea rekodi waliyoiweka miaka 20 iliyopita kwa kuwavua ubingwa, mabingwa wa wakati huo, Zamalet ya Misri, inataka kupata heshima hiyo kwa mara nyingine tena kwa kumalizika ugenini.

Kikubwa Nipashe inazikumbusha Simba na Yanga kuwaheshimu wapinzani wao, kutobweteka na kutumia vizuri kila nafasi ambayo wataitengeneza kwa ajili ya kutafuta matokeo chanya, ushirikiano wa wachezaji utasaidia timu kufikia malengo, zaidi kupata matokeo mazuri kwenye dakika 90 za kwanza.

Wachezaji wa Simba na Yanga wanatakiwa kufahamu hili ni daraja lao lingine la kutangaza vipaji vyao kwa sababu hatua ambayo wamefikia ni kubwa, mawakala na makocha mbalimbali ndani na nje ya Afrika watakuwa wanafuatilia michezo hiyo kwa ajili ya kuboresha na kuimarisha vikosi vyao kuelekea msimu ujao.

Ni wakati mwingine muhimu kwa nyota wa Kitanzania ambao wamekuwa na wakati mzuri kama Mzamiru Yasin wa Simba na Dickson Jon wa Yanga, kuwavutia makocha wa kimataifa kuwasajili kwa sababu mafanikio watakayopata mbali na kunufaika na fedha za usajili, watarejesha nguvu zao katika kuisaidia Timu ya Taifa (Taifa Stars), kufanya vyema.

Bado ndoto za wachezaji wengi wa Tanzania kupata fursa ya kucheza soka la kulipwa hazijatimia, tutumie nafasi hii kama daraja na hatimaye msimu ujao tushuhudie vijana wetu wakisajiliwa ughaibuni na kuacha Simba na Yanga kutumika kama ngazi kwa nyota wageni kuelekea Ulaya.


Hakuna kisichowezekana, kama wachezaji wa Simba na Yanga watapambana vyema katika dakika zote 180, wanaweza kumpa heshima ya kipekee Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan ya kutinga robo fainali, fainali na hata kubeba ubingwa wa Afrika kwa mara ya kwanza.

Katika mechi za nyumbani, mashabiki jitokezeni kwa wingi kuwapa hamasa wachezaji wetu, mkishangilia kwa heshima hadi lengo la kila timu litimie.

Kila la kheri Simba, kila la kheri Yanga. Mungu ibariki Tanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Simba, Yanga huu ni wakati wenu Afrika

**KUANZIA** leo, macho na masikio ya mashabiki wa soka nchini yataelekezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na Uwanja wa Godswill Akpabio nchini Nigeria kwenye mechi za kimataifa hatua ya robo fainali ambapo timu za Simba na Yanga zitacheza.

Nchini, wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, Simba, itacheza na Mabingwa wa Afrika, Wydad Athletic Club, maarufu kama Wydad Casablanca, wakiwa kwenye kampeni yao ya kuwania tena ubingwa kwa mara ya pili.

Wakati Simba wakiwa nchini, Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga wakiwa ugenini nchini Nigeria kucheza dhidi ya Rivers United kwenye mechi ya Kombe la Shirikisho hatua kama hiyo hiyo ya robo fainali.

Ni mechi kubwa na muhimu kwenye historia ya soka la Tanzania kwani hakuna rekodi yoyote inayoonyesha kuwa timu zote mbili zimeshawahi kufikia hatua kama hiyo kwa pamoja, japo kwenye michuano miwili tofauti.

Wakati Simba ikifika hatua hiyo mara tatu kwenye Ligi ya Mabingwa na Shirikisho Afrika mara moja, Yanga ilikuwa ama haishiriki, au inatolewa mapema.

Naweza kusema tangu soka la Tanzania lianze huu ndiyo msimu bora zaidi kuwahi kutokea kwenye historia ya soka la nchi hii.

Kinachotakiwa tu ni kwamba kiwango kilichoonyeshwa na timu hizo msimu huu kiwe na muendelezo.

Yapo maneno ya kuzikatisha tamaa timu hizo za Tanzania kuonekana kuwa zinapambana na timu ambazo ni bora zaidi yao na hazitoweza kufanya kitu chochote.

Unakuta maneno haya ni wa baadhi ya wachambuzi wa soka, ambao badala ya kuzipa moyo na nguvu wanazikatisha tamaa na kuzitisha.

Hatusemi wawe wanazisifia, la hasha, ila wao kama wanahabari wanatakiwa kutafuta uzuri na ubaya ya wapinzani wa timu za Tanzania kwa ajili ya kuzitahadharisha kuwa ziwe makini upande huu ambao wapinzani wapo vizuri na watumie mapungufu haya.

Mfano kusema Simba ni ngumu kuifunga Wydad Casablaca si kweli. Ukweli unabaki pale pale kuwa mechi ni ngumu, lakini soka ni mchezo wa kimbinu ambapo lolote linaweza kutokea kama kocha amemzidi mwenzake mbinu kwa siku hiyo.

Simba ilishawahi kucheza na Sevilla ya Hispania hapa nchini mwaka 2019, japo ilifungwa mabao 5-4, lakini ilikaribia zaidi kushinda kama si Kocha Mkuu wakati huo, Patrick Aussems kuanza kuwaingia wachezaji wa akiba wote, ili mradi tu kila mchezaji aweke rekodi ya kucheza na timu hiyo kubwa kabisa barani Ulaya na duniani kwa ujumla.

Timu hiyo ilishawahi kuifunga Al Ahly, wakiwa mabingwa wa Afrika mara mbili kwenye michuano hii hii ya Ligi ya Mabingwa na hata mwaka 1984, Simba ilishinda mabao 2-1 Uwanja wa CCM Kirumba.

Wakati huo Al Ahly walikuwa ni mabingwa wa Afrika, wakiwa na mchezaji bora wa Afrika wakati huo, straika hatari Mohamed El Khatib.

Mwaka 2003, Simba ilitoa Zamalek kwa namna ambayo haikutarajiwa, kwani baada ya kushinda bao 1-0 nchini ilitegemewa kwenda kufungwa mechi ugenini, lakini ilifungwa bao 1-0 na ikaivua ubingwa wa Afrika kwa mikwaju wa penalti.

Hivi majuzi tu, Simba ilicheza mechi ya kirafiki dhidi ya CSKA Moscow ya Urusi kwenye mechi ya kirafiki ya kimataifa.

Hiyo ni mfano michache inayoonyesha kuwa siyo Simba tu, hata Yanga inaweza kushinda mechi za robo na kutumbukia hatua ya nusu fainali kwani soka siku zote halitabiriki.

Kingine ni kwamba Simba na Yanga na mashabiki wao wasiogope au kutishwa kucheza na timu yoyote ile kama kweli zina nia ya kutaka kutwaa makocha haya makubwa.

Nimekua nikiwasilia Simba wakisema wanalitaka taji la Ubingwa wa Afrika. Kama wanalitaka wanatakiwa wasitishwe au kuogopa na timu yoyote ile.

Ukishafika hatua kama hizi hakuna timu nyonge au ya kawaida tena. Zote zinakuwa timu ngumu na mara nyingi zimeshatwaa ubingwa huu.

Kwenye hatua hii huwezi kuchagua timu au kusema afadhali ya timu fulani. Ili kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa na kufika hatua za mwisho au kutwaa ubingwa inabidi uzifunge timu bora. Huwezi kuwa timu bora wakati hujakutana na timu ngumu na kuzifunga timu bora. Kila la kheri wawakilishi wetu.

## HABARI KITAIFA

# Kituo cha biashara kutoa ajira 15,000

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, juzi alizindua ujenzi wa Kituo cha Biashara cha Afrika Mashariki na Kati ambacho ni cha aina yake kitakachokuwa na maduka 2,000 na kinatarajiwa kutoa ajira 15,000 za moja kwa moja.

Baada ya kukamilika, kituo hicho kitawezesha nchi za Afrika Mashariki kununua bidhaa za China hapa nchini.

Kituo hicho kinachojengwa kilipokuwa kituo cha mabasi Ubungo Terminal kinamilikiwa na Kampuni ya China ya East Africa Commercial & Logistics Center na kitagharimu Dola za Marekani milioni 100.

Akizungumza wakati wa ufunguzi huo, Majaliwa alisema kituo hicho ni cha kimkakati kwa kuwa kitakuwa na maduka makubwa na madogo na kitasaidia kwa kiwango kikubwa kukuza uchumi. Alisema licha za ajira za moja kwa moja, kituo hicho kinatarajiwa kutoa ajira za muda zipatazo 50,000 kwa wananchi wa Dar es Salaam.

Alisema kituo hicho kitapanua fursa kwa Watanzanjia wengi ambapo wafanyabiashara wadogo wadogo, maarufu kama machinga, nao watapata nafasi ya kufanya biashara nje ya jengo hilo.

Waziri Mkuu alisema maduka hayo yatakuwa na bidhaa za nyumbani, zana za kilimo, nguo na bidhaa mbalimbali za viwandani na aliwapongeza kwa ubunifu mkubwa walioufanya kwa kuanzisha kituo hicho ambacho kiko eneo la kimkakati kwa kuwa bararaba nyingi zinakutana hapo, hivyo ni rahisi kufikika.

"Ubungo inafikika kutoka Mbagala, Gongolamboto, Mbezi, Kariakoo, Kivukoni na maeneo mengine. Nitoe wito kwa wakazi wa Dar es Salaam kuongeza miundombinu.

Kama kutakuwa na maduka 2,000 ina maana wananchi wa nchi jirani za Rwanda, Burundi na Congo DRC , Malawi, Msumbiji na Zambia watakuja kufanya manunuzi (ununuzi) hapa kwa hiyo hizi nyumba za kulala wageni hapa hazitatosha ongezeni," alisema.

Alisema uhusiano wa Tanzania na China ulioasisiwa na viongozi wa mataifa hayo mawili, utaendelea kuimarika kwa miaka yote na aliwataka wafanyabiashara kutoka nchi hiyo kuendelea kuwekeza kwenye biashara mbalimbali kwani serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri.

"Napenda kuwathibitishia ndugu zangu wa Jumuiya ya wachina walioko hapa nchini kwamba uhusiano wetu utaendelea kuimarika kwa hiyo wanakaribishwa kuendelea kuwekeza kwenye nyanja mbalimbali kwani tunaendelea kuweka mazingira rafiki ya biashara," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali imeendelea kuimarisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kwa kuboresha kituo chake cha mahala pamoja wateja ili kuvutia zaidi uwekezaji kwa kupunguza kero na hali hiyo imesababisha ongezeko la usajili wa miradi. Alibainisha kuwa kati ya mwaka 2021 na 2023, serikali imesajili miradi 537 ambayo inatarajiwa kutoa zaidi ya ajira 92,900.

Mkurugenzi Mtendaji wa East Africa Commercial & Logistics Center, Cathy Wang, alisema ujenzi wa kituo hicho ulipangwa uanze mwaka 2015 lakini ndoto hiyo imekamilika na mradi kuanza utekelezaji mwezi Desemba mwaka jana.

"Tulipitia changamoto mbalimbali kufika hapa tulipo sasa. Hata hivyo, tunasema kile kilicho na thamani kuwa nacho ni bora kusubiri katika miaka hii. Hatukukata tamaa bali tumejitahidi kusonga mbele na lengo kuu ni kuendelea kuchangia katika kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na China," alisema.

Alisema kampuni yao imedhamiria kujenga kituo hicho cha kimkakati kitakachoongoa Afrika Mashariki kwa ajili ya bishara za huduma na bidhaa kwa kunakili bidhaa za China kwenye soko la Yiwu na Dubai DragonMart na kuzileta hapa Tanzania.

Alisema kituo kitawezesha kukuza biashara ndogo nchini na kupanua biashara hizo ndani ya soko kubwa la Afrika.

Kuhusu kuagiza bidhaa na kuuza bidhaa nje ya Tanzania ikiwepo mazao ya kilimo ya Tanzania, alisema kampuni hiyo imewezesha kufanikisha mazao kama soya, kahawa, mbao, Korosho, ufuta, bidhaa za uvuvi na mvinyo kuuzwa China na wakati huo huo wakiagiza bidhaa zenye ubora wa hali ya juu kutoka China kwa ajili ya soko la Tanzania na Afrika kama mitambo ya kilimo, nguo na vipuri vya mitambo.



Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, SF Kamila Labani akitoa tahadhari kwa viongozi wa serikali ya mtaa wa Mkapa, kata ya Igoma jana, kuhusu uuzaji wa viwanja holela katika maeneo ya milimani, baada ya Jeshi hilo kwa kushirikiana na serikali ya Wilaya ya Nyamagana, kufanikiwa kulipasua jiwe kubwa lililokuwa likitishia usalama wa wakazi wa eneo hilo. **PICHA: VITUS AUDAX.**

# Kairuki akabidhi magari 25 kwa maofisa wa elimu wilaya

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amekabidhi magari 25 ikiwa ni sehemu ya magari 200 yaliyoagizwa kupitia Mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) kwa ajili ya maofisa elimu sekondari wa halmashauri zote nchini.

Pia ameahidi kujenga bweni la wanafunzi wa kiume katika Shule ya Sekondari Kibasila ikiwa ni ahadi kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza juzi Dar es Salaam katika hafla ya ugawaji wa magari hayo, Kairuki aliagiza Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA) kukamilisha upatikanaji wa magari mengine 105 yaliyosalia kwa ajili ya maofisa elimu hao.

"Katika halmashauri 184 zinazotakiwa kupata magari, 51 tayari zimepata katika awamu ya kwanza, awamu ya pili 19 na hii awamu ya tatu magari 25, hivyo bado magari 105 kwa maofisa hao," alisema.

Aidha, aliahidi kuwa serikali itaendelea kuboresha elimu na maslahi ya walimu nchini hivyo aliwataka maofisa hao wawe wabunifu kusimamia shughuli za kielimu na kuhakikisha kuwa ubora wa elimu unaimarika.

Kairuki alisema elimu ya sekondari inahitaji uwajibikaji na huwezi kupata mafanikio pasipo kuwa na ubunifu na bidii kwa watumishi hivyo serikali inaendelea kufanya maboresho lakini pia wasimamizi nao watekeleze wajibu wao.

Aliwataka maofisa hao kutumia magari hayo kuongeza ufanisi wa shughuli za kielimu na pia yatunzwe ili yadumu kwa muda mrefu.

Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Abdul Maulid, aliishukuru TAMISEMI kwa kutoa magari hayo kwa sababu yamekuwa yakiwasaidia katika ufuatiliaji wa elimu.

# Zimamoto wafanikisha kusambaratisha jiwe hatarishi bila madhara

**Na Vitus Audax, MWANZA**

JESHI la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza kwa kushirikiana na serikari ya Wilaya ya Nyamagana limefanikisha kufikisha wataalamu wa uchorongaji miamba kutoka migodi ya uchimbaji madini Geita na kusambaratisha jiwe kubwa lililokuwa likitishia maisha ya wakazi wa mtaa wa Mkapa, baada ya kuanza kuhama nafasi yake ya asili kwenda kwenye makazi ya watu.

Hivi karibuni, Nipashe iliripoti uwapo wa jiwe hilo lililokuwa likitishia amani ya wakazi wa Mtaa kutokana na ukubwa wake endapo lingeanguka katika makazi yao na kusababisha madhara, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoa baada ya kupokea taarifa, walifika katika eneo la tukio na kuona hali ya jiwe hilo na kushirikisha uongozi wa wilaya ili kupata wataalamu wa kulisambaratisha bila kuleta madhara.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, Mrakibu (SF) Kamila Labani, alisema kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana waliwapeleka wataalamu wa miamba na kusambaratisha jiwe hilo bila kuleta madhara kwa makazi ya watu wala mtu yeyote.

"Jiwe lilikuwa katika eneo baya la mteremko na muda wowote lingeangukia makazi ya watu lakini tumefanikiwa kulisambaratisha, hivyo wananchi wanatakiwa kuacha kuchokonoa mawe ya aina hii maana tulikuta jiwe hili limepasuliwa upande mmoja na kusababisha lianze kuhama nafasi yake," alisema SF Kamila

Alisema kazi ya kupata wataalamu hao na kemikali za kulisambaratisha jiwe hilo zimeigharimu serikali fedha nyingi ambazo zingefanya shughuli zingine za maendeleo, hivyo kutoa rai kwa wananchi wanaochimba mchanga holela na kupasua mawe bila utaratibu, kuomba vibali kwa uongozi wa serikali za mitaa ili wahakikishe kuwa ni salama kufanya hivyo.

Baadhi ya wakazi wa eneo hilo, waliomba serikali kuendelea kudhibiti upasuaji wa mawe makubwa holela hususani katika makazi ya watu waliojenga milimani ili kuondoa hofu na hasara za mara kwa mara.

"Tunashukuru Nipashe kwa kufuatilia suala hili lilokuwa likitutia hofu hasa kwa watoto wetu wanaochezea mazingira haya lakini kwa sasa limetatuliwa. Tunaishukuru pia serikali kupitia Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulichukulia umakini suala hili mpaka limetatuliwa tunaomba waendelee kudhibiti watu wanaopasua miamba holela," alisema Frida Ramadhani.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Fadhil Emmanuel, aliahidi kuendelea kufuatilia nyendo za wananchi wa mtaa huo hususani katika kupasua mawe na kuchimba mchanga holela na kuhakikisha nadhibiti vitendo hivyo ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza.

# Mambo 7 yatajwa kichocheo kwa watoto kuishi mitaani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UTAFITI uliofanywa na serikali katika mikoa sita ya Tanzania Bara umebainisha sababu za watoto kuishi na kufanya kazi mitaani huku idadi yao ikipungua kutoka watoto 6,393 mwaka 2017/18 hadi 4,383 mwaka 2020/21.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mwanaidi Ali Khamis, alisema hayo juzi bungeni, alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Tamima Haji Abbas.

Mbunge huyo alitaka kujua kama kuna utafiti uliofanywa na serikali kujua sababu za kuwapo watoto wa mitaani.

Akijibu swali hilo, Mwanaidi alitaja mikoa sita iliyofanyiwa utafiti ni Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Arusha na Iringa. Alisema miongoni mwa sababu walizobaini ni malezi duni, yatima na migogoro katika familia.

Naibu Waziri alitaja sababu zingine zilizogunduliwa ni shinikizo la makundi rika, ukatili na unyanyasaji majumbani, umasikini wa kipato katika familia na utumikishaji wa watoto mijini.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alitaka kujua mpango wa serikali kukabiliana na tatizo la watoto wa mitaani baada ya kubaini kiini chake.

Naibu Waziri Mwanaidi, akijibu swali hilo, alisema serikali itaendelea na mikakati endelevu ya kutoa elimu ya malezi bora kwa wazazi na matunzo ili kuwatunza watoto katika ngazi familia na itakutanisha watoto na wazazi wao.

Alisema kwa watoto ambao hawana wazazi, watapata huduma na haki zote stahiki kupitia vituo vya kulea watoto cha Dodoma, Kikombo na Kurasini mkoani Dar es Salaam na kuimarisha ulinzi na usalama kwa watoto hao.

"Kama serikali tunaahidi kuendelea kufanya utafiti mbalimbali katika mikoa ambayo ina changamoto za watoto wa mitaani lakini pia kuhakikisha usalama wao," alisema.

Alitoa rai kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanakaa na watoto wao ili kupata malezi bora na kuwakumbusha "mtoto wa mwenzio ni wako na wanastahiki kupata haki stahili kwa kuwa mtoto wa leo ni taifa la kesho".

Tanzania ina Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na imesharidhia mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ya kuhakikisha kunakuwa na ulinzi kwa watoto ili wakue na kulelewa katika mazingira salama.



Mratibu wa Udhibiti wa Malaria Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Ford Chisongela (kulia), akitoa ufafanuzi juu ya malaria wakati wa semina ya waandishi wa habari na mpango wa taifa wa kudhibiti malaria, mkoani humo jana. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# DAWASA yaanza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu

**Na Joseph Mwendapole**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), imeanza kupanda miti katika maeneo ya hifadhi za miundombinu ya maji ili kutunza vyanzo vya maji ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Meneja wa Mkoa wa Kihuduma wa DAWASA Mabwepande, Haruna Taratibu, alisema juzi kuwa kupanda miti kwenye eneo hilo ni hatua mojawapo ya kutunza mazingira na vyanzo vya maji pamoja na kuzuia mmomonyoko wa udongo hatimaye kuboresha mwonekano wa maeneo ya kutolea huduma za maji.

"Pamoja na agizo la Waziri Mkuu kuzitaka taasisi na wananchi wote kwa ujumla tupande miti rafiki wa mazingira. Sisi DAWASA mkoa wa kihuduma Mabwepande, tumeona tuje kupanda miti katika eneo hili la tangi la Malolo ili kuboresha mazingira ya hapa na kutunza chanzo chetu cha maji," alisisitiza.

Alisema zaidi ya miti 1,000 imepandwa na watumishi wa mamlaka hiyo ikiwamo miti ya matunda, kivuli na maua katika maeneo mbalimbali ya kihuduma ya mamlaka.

Wakati huo huo, zaidi ya wakazi 300 wa kata ya Mbezi, wilaya ya Ubungo, wameachana na matumizi ya maji chumvi waliyokuwa wakiyatumia kupitia mradi wa maji wa jamii Mpiji Magoe katika kata hiyo.

Hatua hiyo inatokana na DAWASA kukabidhiwa mradi huo wa jamii na kuunganisha katika mtandao wa majisafi wa mamlaka.

Akizungumzia utekelezaji wa mradi huo, Mhandisi wa Miradi wa DAWASA Mabwepande, Adam Makinda, alisema wananchofanya kwa sasa ni kuwatembelea wateja pamoja na kuwabadilishia mita za zamani ili kuingia rasmi kwenye huduma za DAWASA.

"Wakazi hawa wametumia maji chumvi kwa muda mrefu, lakini sasa wote wanakwenda kupata maji ya DAWASA, zoezi la upimaji limekwisha anza na zaidi ya wateja 120 wameshajaza fomu kupatiwa huduma," alisema.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kibesa, Said Diuchille, aliishukuru DAWASA kwa kuwatoa wananchi wake katika matumizi ya maji chumvi na sasa wana uhakika na afya zao kwani wanaenda kutumia majisafi na salama.

Henry Ngumuo, mkazi wa mtaa wa Igoma, aliishukuru serikali kupitia DAWASA kwakuona umuhimu wa kuwaondolea adha ya matumizi ya maji chumvi na kuwaletea majisafi.

"Maji chumvi hayakua mazuri kwa afya zetu lakini pia ilituwia vigumu kuyatumia kwa kila matumizi ya nyumbani, maji haya ya safi na salama kwetu ni neema, tupo tayari kutoa ushirikiano wa kila namna kwa DAWASA" alisema.

Mradi wa maji wa jamii kata ya Mbezi zamani ulijumuisha jumla ya vizimba 11 vya kuchota maji na kuhudumia eneo la Mbezi mitaa ya Mpiji Magoe, Mpiji Center, Kibesa, CCM ya Zamani, Uzunguni na Igoma ambao wote watanufaika na maji safi ya DAWASA.

# Ujenzi wa barabara Uvinza-Malagarasi kukamilika Oktoba

**Na Mwandishi Wetu,** KIGOMA

SERIKALI kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), imesema ujenzi wa barabara ya Malagarasi-Ilunde-Uvinza yenye urefu wa kilometa 51.1 kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 31 na unatarajiwa kukamilika Oktoba, mwaka huu.

Kaimu Meneja wa TANROADS Mkoa wa Kigoma, Mhandisi Ngoko Mirumbe, alisema hayo juzi wakati wa ziara ya waandishi wa habari katika miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa mkoani hapa.

Alisema serikali imelenga kuhakikisha inaiunganisha mikoa yote nchini kwa barabara za lami, jitihada ambazo zinajidhihirisha kwa uwapo wa miradi mingi ya ujenzi wa barabara za lami ndani ya mkoa wa Kigoma, hivyo kurahisisha usafiri na usafirishaji ili kuchangia uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.

"Ujenzi wa barabara hii ni moja ya uwapo wa miradi mbalimbali inayoendelea kutekelezwa kwa kasi ndani ya mkoa ambayo inaashiria ndani ya muda mfupi sana kutoka sasa, mkoa wa Kigoma utakuwa umeshaunganishwa kwa miundombinu ya barabara za kiwango cha lami," alisema.

Mradi wa Malagarasi - Ilunde - Uvinza, alisema ni sehemu ya barabara kutoka Kigoma-Uvinza-Malagarasi yenye urefu wa kilometa 212. Kilometa 105 kutoka Kigoma hadi Uvinza zimeshajengwa kwa kiwango lami tayari na sasa hadi kuelekea Tabora zimesalia kilometa 61 ambazo zote mkandarasi yuko kwenye eneo la ujenzi.

Alisema ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami unagharimu zaidi ya Sh. bilioni 62 na mradi unatekelezwa kupitia mkandarasi STECOL Cooperation chini ya Mhandisi Mshauri Norplan Tanzania

Aidha, amebainisha kuwa mradi umeajiri wafanyakazi 216 kati yao wafanyakazi wageni wakiwa ni 21 pekee.

Kaimu Mhandisi Mkazi, Mhandisi Yusuf Karera amesema, hadi sasa kazi mbalimbali za utekelezaji wa mradi huo zimefanyika ikiwemo kujenga makaravati 22 huku makaravati madogo yakiwa ni 19 na makaravati makubwa matatu.



## DC akemea vitendo vya ushoga, usagaji wilayani kwake

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali, amekemea uwapo wa vitendo vya ushoga na usagaji wilayani humo na kuwataka wananchi kusimama katika misingi ya imani na utamaduni wa mtanzania.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi wa kata za Tumuli na Msingi, alipofanya ziara ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Machali alisema haki za binadamu hazipatikani kwa kufanya vitendo ambavyo ni kinyume na mapenzi ya Mungu.

"Niwaombe viongozi wangu wa dini mliopo hapa hakikisheni kwenye nyumba zenu za ibada mnapinga kwa nguvu zote vitendo hivi ambavyo vinabadili utamaduni wetu," alisema.

Alisema katika kipindi hiki ambacho mambo mabaya yanajitokeza wazazi wanapaswa kutumia muda mwingi kuongea na watoto kuhusu madhara ya ushoga na usagaji ili kuwa na kizazi chenye maadili mazuri.

Aidha, aliwataka wananchi hao kuhakikisha wanashiriki katika shughuli za maendeleo zinatolewa na serikali na kutoa ushirikiano katika kuwabaini wahalifu wote ambao wanatishia amani katika wilaya hiyo.

Aliwataka wakuu wa idara na taasisi mbalimbali wilayani Mkalama kuhakikisha wanashughulikia kero na kutatua migogoro yote hususani ya ardhi na mipaka ili wananchi wawe wanatumia muda mwingi kwenye masuala ya maendeleo badala ya migogoro isiyo na tija.

# Askofu EAGT ataja dawa kukomesha ushoga

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Evangelistic Assemblise of God Tanzania (EAGT), Dk. Brown Mwakipesile amesema tatizo la ushoga na ndoa za jinsia moja siyo la kuinyooshea serikali kidole bali ni wajibu wa kila mtanzania kukemea na kupinga kwa nguvu zote vitendo hivyo.

Aliyasema hayo alipokuwa akizungumza kwenye kongamano la maombi la wanawake waombolezaji lililofanyika mkoani Dodoma ambapo aliwataka Watanzania kusimama kwa nafasi zao kulikemea jambo hilo ikiwa na pamoja kuomba na kufunga ili Mungu aliponye Taifa.

"Tatizo hili siyo la kuiachia serikali peke yake bali linatakiwa kushirikiana kwa pamoja kati ya viongozi wa dini huku tukichukua hatua zinazoweza kuwaokoa hao ambao wanaojihusisha na uovu huo wa ndoa za jinsia moja, ushoga na ukatili wa mauji ya watu wasiokuwa na hatia wakiwemo wanawake watoto na wenye ulemavu. "Maombi ni mali ghafi ya kutoka mbinguni pia ni kombora kwa watenda dhambi, hivyo niwaombe nyinyi wanawake waombolezaji endeleeni kuiombea nchi pamoja na viongozi wa serikali ili Mungu atuepushe na majanga ambayo yamekuwa yanatia hasara kwa jamii na taifa kwa ujumla"alisema

Aidha, aliwataka Watanzania kuendelea kuwaombea viongozi wa serikali ili waiongoze nchi kwa kuzingatia maadili ya kimungu.

Pia, aliyaomba madhehebu ya dini kusimama kwa uaminifu na uadilifu wa kiroho ambao utakaofanikisha kuondoa aibu iliyopo ya ushoga na ndoa za jinsia moja.

Alisema Watanzania wanatakiwa kuomba kwa kila eneo likiwemo Bunge lililopo kwa hivi sasa ili maamuzi yatakayotolewa yawe sahihi kwa faida ya taifa likiwemo suala la ufisadi ambalo limetikisa nchi kwa baadhi ya watendaji wa serikali kutokuwa waaminifu na rasilimali watu na kujiona kuwa wao ndiyo wanaostahili kumiliki na kutumia.

Mwenyekiti wa Shirika la Maendeleo ya Wanawake Tanzania Mchungaji, Dk. Assumpter Mshama alisema wanawake wakichukua nafasi zao kwa kuomba na kufunga hakuna kitakachoshindikana mbele za Mungu, hivyo hata ushoga, ndoa za jinsia moja na vitendo wanavyofanyiwa kinamama na watoto vinaweza kutoweka.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson akizungumza na wajumbe wa kamati teule ya Rais ya kutathmini ufanisi na utendaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, wakiongozwa na Mwenyekiti wake, Balozi mstaafu Hassan Yahya (kulia kwake), walipomtembelea Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Jafo ahimiza kulindwa miundombinu ya miradi

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amewataka wananchi kushirikiana na serikali kulinda miundombinu ya miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi inayotekelezwa na mashirika na taasisi mbalimbali.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi wa Kata ya Ugogoni na Sejeli Wilaya ya Kongwa kwenye uzinduzi wa mradi wa josho la kuogeshea mifugo iliyotekelezwa na Shirika la Foundation for Energy Climate and Change kwa kushirikiana na halmashari hiyo.

Alisema miradi hiyo iliyotekelezwa na mashirika na taasisi hizo ina gharimu fedha nyingi, hivyo wananchi wanatakiwa kuilinda miundombinu yake ili iweze kuhimili mabadiliko yake ya tabianchi, badala ya kuiachia serikali peke yake.

Akizungumza na wananchi wa kata hizo alisema kuwa amefurahishwa na utekelezaji wa mradi huo wa josho la kuogeshea mifugo, hivyo akawataka wasimamizi kukamilisha uwekaji wa miundombinu ya maji ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Awali akitoa taarifa kuhusu mradi huo, Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Kongwa, Msafiri Mkunda, alisema kuwa ujenzi wa josho hilo lenye ujazo wa lita 12,000 umekamilika na shughuli za kuogesha mifugo zinafanyika kwa asilimia 90.

Alisema kuwa wananchi kupitia kamati ya uendeshaji, wamejiwekea utaratibu maalumu wa kuendesha josho hilo ambapo kwa kuchangia ng'ombe mmoja shilingi mia na shilingi hamsini kwa mbuzi na kondoo na uchangiaji huo ni kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa dawa.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel aliwataka wananchi kushirikiana na viongozi wa halmashauri ili kuisimamia vizuri miradi kwa lengo ya kuiwezesha miundombinu yake kudumu.

"Wananchi wa kata hizi mbili tuna kila sababu ya kuishukuru serikali kwa kutujengea mradi huo ambao kwa hivi sasa tunaamini kuwa wananchi watakula nyama salama inayotokana na mifugo salama iliyotibiwa kiafya kutoka na josho hili,"alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Machenje, Hamis Lechipya alishukuru serikali kwa ujenzi wa josho hilo akisema litawaletea manufaa baada ya wananchi kukosa huduma hiyo ya kuogesha mifugo yao kwa kipindi kirefu.





# Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi Sikukuu ya Eid-El-Fitri

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR.**

JESHI la Polisi Zanzibar limesema litahakikisha linaimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao hasa katika kipindi hiki cha Sikukuu ya Iddi-El- Fitri ambapo vitendo vya uhalifu huwa vingi.

Akizungumza na waandishi wa Habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, ACP Richard Thadei Mchomvu alisema jeshi hilo halitosita kuwachukulia hatua kali za kisheria watu watakaojihusisha na viashiria vya uvunjifu wa amani katika kipindi chote cha sikukuu hiyo.

Alisema jeshi hilo limejipanga kuimarisha ulinzi na usalama katika kipindi chote hicho ikiwemo viwanja vya sikukuu, usalama barabarani, doria na misako, pamoja na maeneo mengine ili kuona wananchi wanasherehekea sikukuu hiyo kwa amani na utulivu.

Alisema wapo baadhi ya watu hutumia sikukuu hiyo kama chanzo cha kuvunja amani ya nchi, kufanya vitendo viovu na kujipatia kipato kwa njia isiyo halali hivyo haitasita kumchukulia hatua kali pale atakapokamatwa.

Aidha, walisema katika kuimarisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama viitafanya doria na misako katika maeneo mbalimbali kwa muda wote wa kipindi cha sikukuu.

"Kutakuwa na askari wa vitengo wa kutosha kwenye viwanja vya sikukuu pamoja na kuimarisha doria za magari, doria za miguu vilevile na kikosi cha mbwa na farasi kitatumika ili kuhakikisha usalama wa raia na mali zao unaimarishwa hadi kumalizika kwa sikukuu hiyo," alisema.

Kamanda Mchovu aliwataka wananchi wanapotoka majumbani kwenda kwenye viwanja vya sikukuu kuhakikisha hawaziwachi nyumba bila ya mtu, kuepuka kuwavisha watoto wao vitu vya thamani na kutotembea peke yao.

Alisema hali hiyo husababisha baadhi ya wananchi hutumia mwanya wa sikukuu kuvunja nyumba na kuiba pamoja na kupora na kuwanyang'anya mali zao.

Kuhusu usalama, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kusini Unguja ASP Gaudianus Kamugisha alisema kutakuwa na askari katika barabara zote kwa muda wote wa sikukuu ili kudhibiti madereva wazembe na wasiotaka kutii sheria za usalama barabarani.

Hivyo, waliwaomba madereva wa vyombo vya moto kuwa na tahadhari wanapoendesha vyombo hivyo kwa kuzingatia sheria ili kuepusha ajali.

Waliwaasa wananchi kusherehekea sikukuu hiyo kwa amani na utulivu na sikukuu isiwe chanzo cha kufanya vitendo vya uvunjifu wa amani ikiwemo, wizi, uporaji, unyanganyi, udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia.



Baadhi ya wananchi wakiwa katika harakati za kuchinja ng'ombe, kwa ajili ya maandalizi ya Sikukuu ya Eid El Fitr, jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kiwanda cha ZMC chalaani tabia kughushi vifungashio

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MENEJA wa Kampuni ya Zanzibar Milling Corporation, Rehema Salim, amesema kitendo cha utapeli kinachofanywa na baadhi ya watu kughushi vifungashio vya kampuni hiyo ni kinyume na sheria za biashara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake kuhusu uwapo wa udanganyifu wa bidhaa hiyo ya unga wa ngano alisema wamebaini uwapo wa vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya watu kughushi baadhi za unga wa ngano wa Azam ukiwemo unga wa bekari unaojulikana kama Azam boflo.

Alisema wamefanya utafiti na kugundua kuwa baadhi ya watu wananunua viroba vilivyotumika vya unga wa Azam na kuweka unga tofauti usio na ubora.

Alibainisha kuwa bidhaa hizo za kughushi ambazo zipo chini ya kiwango huhifadhiwa tena kwa kutumia viroba vya Azam vilivyotumika na kuuzwa zikiwa na chapa ya Azam jambo ambalo huwapotosha watumiaji na kuamini kuwa wanunua bidhaa halisi ya Azam.

Rehema alisema bidhaa za unga wa ngano wa Azam zimefungwa katika mifuko maalum yenye nembo ya kampuni na alama mbalimbali za utambulisho wa ubora unaotambulika na Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS).

Alisisitiza kwamba kampuni hiyo inashirikiana na mamlaka husika ili kuwabaini watu wanaofanya uhalifu huo na kutoa zawadi ya Sh. milioni moja kwa yoyote atakaetoa taarifa inatakayosababisha kukamatwa kwa wahalifu hao na bidhaa zilizoghushiwa. Pia aliwaomba wateja wake kuendelea kuwaunga mkono na kuamini bidhaa zao na kuwahakikishia kwamba kampuni itaendelea kuzalisha bidhaa bora na salama.

Meneja Uzalishaji wa kiwanda hicho, Yahya Makihehebu Tuli, alisema matukio hayo kwa Zanzibar ni mara ya pili watu kufanya hivyo, lakini wamekuwa wakiyapatia ufumbuzi kwa kubadilisha aina mbalimbali ya vifungashio ili kuepuka matatizo hayo. "Tumepokea malalamiko kutoka kwa wananchi na wafanyabiashara wanaotengeneza mikate ya boflo ambao hutumia unga wetu kuwa Unguja wanaotumia hauna ubora na bidhaa zao kuharibika,"alisema.

Aidha, aliwaomba wafanyabiashara ambao wananunua unga kwa jumla kufika kiwanda cha Azam na wale wanaonunua kwa wauzaji wa jumla kuhakikisha wananunua kwa wauzaji ambao wanafahamika ambao wanachukua unga katika kiwanda hicho.

Akizungumzia uzalishaji wa kiwanda hicho alisema huingiza sokoni mifuko 2,000 ya kilo 50 ya unga wa ngano wa boflo.

Alisema kiwanda chao kina uwezo wa kuzalisha tani ya ngano ghafi 350 kwa siku ambapo mahitaji ya Zanzibar kwa siku ni 250.

Hivyo, aliihakikishia serikali kwamba kiwanda hicho kina uwezo wa kulisha Wazanzibar bila ya tatizo lolote kupitia bidhaa yao na kuwaasa tasisi ya viwango kuhakikisha kwamba bidhaa zote zinazoingia nchini basi zinakidhi viwango kwani mtu asingehangaika kughushi kama angeingiza bidhaa yenye viwango.

## Maadhimisho uhuru wa habari kufanyika Zanzibar Mei

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAADHIMISHO ya uhuru wa habari Tanzania kitaifa yanatarajia kufanyika visiwani Zanzibar, kwamba yatawakutanisha wadau wa habari na wanahabari mbalimbali.

Maadhimisho hayo ambayo yanatarajiwa kufanyika Mei, 3 mwaka huu na kufunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussen Ali Mwinyi.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari Mjini Zanzibar, Mwenyekiti wa Mtandao wa Majukwaa ya Vyombo vya Habari Zanzibar, (ZAMECO), Farouk Kareem, alisema maadhimisho hayo ambayo yataambatana na kongamano ni fursa nzuri kwa waandishi wa habari.

Akitoa taarifa ya serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Mkurugenzi wa Habari Maelezo Zanzibar, Hassan Khatib Hassan, alisema serikali inaendelea kuthamini michango ya vyombo vya habari na itaendelea kushirikiana nayo kila siku.

Alisema wageni 300 watashiriki wakiwemo washirika wa maendeleo, waandishi wa habari, jumuiya za kiraia na watetezi wa haki za binaadamu, watafiti na wasomi na wadau wa habari ambapo mada mbalimbali zitajadiliwa na maonyesho mbalimbali yatakuwepo na utoaji wa tunzo kwa waandishi wa habari.

Alisema maadhimisho hayo ni kukuza uelewa wa umuhimu wa uhuru wa vyombo vya habari na kuikumbusha serikali na jamii umuhimu wa kuheshimu na kulinda haki ya uhuru.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania Zanzibar, Dk. Mzuri issa, alisema, maadhimisho hayo yatakuwa na aina yake ambapo serikali hutoa kipaumbele kwa haki ya uhuru wa kujieleza, uhuru wa vyombo vya Habari, usalama wa wanahabari na uhuru wa kujieleza.

Dk. Mzuri, aliishukuru Wizara ya Habari kwa kuona umuhimu wa kufanya marekebisho ya sheria kandamizi za uhuru wa habari ili kuimarisha sekta ya habari pamoja na uhuru wa kujieleza.

Maadhimisho hayo yameandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi.

BUKUNMI
UKURASA 14



Nipashe
BT
BUDANI TELE



# ZOGO TUPU

TASNIA ya filamu imeingia katika zogo kubwa baada ya filamu inayoangazia maisha ya malkia wa Misri, Cleopatra VII, kukabiliana na ubaguzi wa rangi.

Filamu hiyo iliyotolewa na Netflix ambayo inaonyesha Malkia Cleopatra, kama Mwafrika mweusi imezua malalamiko kutoka kwa raia wa Misri wakipinga rangi hiyo.

Tayari mwanasheria mmoja amewasilisha malalamiko yanayowashutumu kampuni ya African Queens, kuwa kumuonyesha Malkia Cleopatra ana rangi nyeusi ni kukiuka sheria za vyombo vya habari na kulenga kufuta utambulisho wa Misri.

Mwanaikolojia mkuu wa nchi hiyo alisisitiza kuwa Cleopatra alikuwa na ngozi nyeupe, sio mweusi.

Lakini mtayarishaji wa filamu hiyo alisema urithi wake unajadiliwa sana.

Mwigizaji wa nafasi hiyo Adele James, amesema ikiwa mtu hapendi uigizaji wake wa mwafrika, asitazame kipindi hicho.

Adele alitoa maoni hayo katika kurasa ya Twitter iliyoangazia maoni mbalimbali ambayo yalionekana ya kibaguzi.

Cleopatra alizaliwa katika jiji la Alexandria nchini Misri mwaka 69 KK na akawa malkia wa mwisho ya watu wanaozungumza Kigiriki iliyoanzishwa na jenerali wa Alexander the Great wa Macedonia Ptolemy.

Alimrithi baba yake Ptolemy XII mwaka 51 KK na kutawala hadi kifo chake mwaka 30 KK..

Utambulisho wa mama yake Cleopatra haujulikani na wanahistoria wanasema inawezekana kwamba yeye, au mtu mwingine wa kale wa kike, alikuwa Mmisri wa kiasili au kutoka kwingineko barani Afrika.

Tovuti shirikishi ya Netflix ya Tudum iliripoti mnamo Februari kwamba chaguo la kumuigiza Adele James, mwigizaji wa Uingereza ambaye ni wa kabila mchanganyiko, kama Cleopatra katika filamu yake mpya ilikuwa ikiashiria mazungumzo ya karne nyingi kuhusu mtawala wake.

Jada Pinkett Smith, muigizaji wa Marekani ambaye alikuwa mtayarishaji mkuu na msimulizi, alinukuliwa akisema: "Si mara nyingi tunapata kuona au kusikia hadithi kuhusu malkia weusi na hiyo ilikuwa muhimu sana kwangu na kwa binti yangu na kwa jamii yangu tu kuweza kujua hadithi hizo kwa sababu zipo nyingi!"

Lakini tangazo la filamu hiyo ilipotolewa wiki iliyopita Wamisri wengi walikasirishwa na taswira ya Cleopatra.

**BBC**

BASI SAWA

## Whozu acha kuwadanganya



MWANAMUZIKI wa Bongo Fleva, Whozu, amekiri kwamba anafurahia kuwa katika mazingira ya Kiislam, ingawa bado hajabadilisha dini.

Amesema mpenzi wake Wema Sepetu na baadhi ya marafiki zake wanamuambia kuwa anapendeza kuwa Muislam hasa kutokana na mazingira anayojiwekea.

"Bado sijabadili dini kuwa muislam, lakini nikiwa katika mazingira haya najisikia raha sana na watu wanaonizunguka wananiambia napendezea, amesema.

## Marioo kwani unamwitaje Diamond?

MWIMBAJI nyota wa Bongofleva, Omari Mwanga, maarufu kama Marioo, amekiri kwa mara ya kwanza kuwa Diamond Platnumz, kuwa kama kaka yake.



Kauli hiyo ameitoa baada ya kuwepo kwa mzozo kutokana na Diamond kueleza msanii huyo aliwahi kutaka kusainiwa kwenye Label ya WCB.

"Kusema ukweli yeye ni Kaka yangu, ni Mtu ambaye mimi namtazamia sana kama kioo na tunaona ambavyo yeye amefanikiwa sana kwenye mziki, kwa hiyo mara nyingi huwa natamani kukaa naye niongee naye kuna uzoefu flani nataka kutoka kwake," amesema.



## VICTOR ANAPOOMBA BARAKA ZA MUNGU

MWANAMUZUKI kutoka Nigeria, Victor Thompson, ameweka wazi kuwa wimbo wake 'This Year Blessings' uliotoka mapema mwaka huu ni zawadi tosha kwa Watanzania.

Akizungumza hivi karibuni, na bosi wa lebo ya Atmosphere Ent, amesema wimbo huo umekuwa baraka ndani na nje ya Nigeria hasa kwa mashabiki wake wa hapa nchini kutokana na kugusa maisha ya watu.

"This Year Blessings ni aina ya wimbo uliofanyika baraka kwangu na mashabiki zangu na k ndani na nje ya Nigeria, hii imenipa nguvu zaidi ya kuendelea kufanya kazi ya Mungu," amesema Victor.





## Mwijaku mdomo utakuponza

MCHEKESHAJI maarufu katika mitandao ya kijamii, Mwijaku amemshauri Marioo kauwa makini na penzi lake jipya aliloingia na mrembo Paula.

Mwijaku amesema, Paula ni mrembo ambaye ana ushawishi wa kipekee na kumfanya mwanamume kutoa kile alichonacho bila matatizo.

"Amuulize mwenzake  jinsi ambavyo anajikusanya sasa hivi, alimalizwa kila kitu sasa hivi ndo kaanza kujikusanya ana milioni 60 tu," amesema Mwijaku

## KOLABO 5 KALI ZILIZOTIKISA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA kwa sasa imekuwa kijiji kwenye nyanja zote hivi sasa.

Hata wasanii wa sasa wana fursa ya kuungana na wenzao kutoka mataifa mbalimbali na kutoa ngoma kwa pamoja.


Mfano msanii wa Bongo anaweza kutoa ngoma na msanii wa Kenya, Uganda au hata nje ya Afrika.

Na hii ni katika kutafuta kile kinachoitwa kubadilisha ladha ya muziki, pamoja na kutafuta kuungwa mkono na mashabiki wengi kwa sababu kwa sasa muziki pia umeingia kwenye mitandao ya kijamii, hivyo kutafuta idadi kubwa ya watu watakaofuatilia kwa kuangalia mtandaoni na hii nayo ni moja ya njia ya kujipatia kipato kwa wasanii kwenye dunia ya leo. Wenyewe wanaita 'kolabo'.

Hapa Tanzania wasanii wengi, mbali na kupiga 'kolabo' na wasanii wenzao wa hapa hapa nchini, lakini pia baadhi wanapiga na wasanii kutoka nje ya nchi.

Baadhi ya wasanii wa Kibongo wameshafanya 'kolabo', na wasanii kutoka nje ya nchi miaka kadhaa nyuma. Leo tunajikumbusha 'kolabo' kazi zilizotikisa huko nyuma.

**Diamond ft Innoss'B-Yope Remix**




Moja ya kolabo bora kuwahi kutokea nchini Tanzania kwenye kipindi zaidi ya miaka mitatu sasa ni hii. Ilileta kitu kipya nchini ambacho ni staili ya uchezaji ambayo iliitwa 'Yope'.

Mwezi Agosti mwaka 2019, msanii wa Kikongomani Innoss'B, alitoa ngoma inayoitwa 'Yope'. Hata hivyo haikuvuma sana. Lakini alipoamua kuungana na Diamond Platnumz na kutoa 'remix' yake mwezi unaofuata Septemba mwaka huo huo ikawa balaa. Wimbo huo uliangaliwa zaidi na kupendwa mno. Ndiyo maana hata leo 'Yope Original' umeangaliwa na watu milioni 56, huku 'remix' yake, ambayo Diamond na Inno wamefanya balaa kubwa umeangaliwa na watu 206 kwenye mtandao wa you tube.

**Harmonize ft Yemi Alade-'Show Me Want You Got'**

Msanii Harmonize amekuwa hashikiki kwa kufanya 'kolabo' za kufa mtu na wasanii mbalimbali wa nje wa nchi, Afrika na nje ya Bara la Afrika.

Moja ya 'kolabo' yake ambayo ameshawahi kuifanya, ni ile ni dhidi ya msanii maarufu wa kike Yemi Alade wa nchini Nigeria.

Kitu ambacho Harmonize amekitoa na Alade ni 'Show Me Want You Got' ambacho kilifyatuliwa mwaka 2019.

**Vanessa Mdee ft Reekado Banks-'Bambino'**

Msanii Vanessa Mdee, ni mmoja wa wasanii wachache wa kike ambao wanafanya sana 'kolabo' na wasanii wa nje ya nchi.

Ameshawahi kufanya 'kolabo' ya nguvu na msanii kutoka Nigeria, Reekado Banks na kutoa ngoma moja kali inaitwa 'Bambino'. hiyo ilikuwa ni 2018.

**Nandy ft Willy Paul-'Hallelujah'**

Nandy naye amekuwa mmoja wa wasanii wa Kibongo ambao wameingia kwenye rekodi ya kupiga 'kolabo' na wasanii wa nje, alipomtafuta Willy Paul wa Kenya na kutoa ngoma moja inayoitwa 'Halleyujah', 2019.

**Diamond ft Koffi Olomode-'Waah'**

Mwaka 2020, Diamond Platnumz alifanya 'kolabo' na mkali wa muziki wa dansi Afrika, Koffi Olomode raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Wakaibuka na ngoma iliyoitwa 'Waah.'

Ni ngoma ambayo nayo ilitikisa, lakini ikikiwa ni kama 'remix' ya wimbo wa Koffi 'Papa Ngwasuma', ambaye wengi wanaufahamu kwa jina la 'Papa Mobimba.'

FILAMU

## Ombi Langu: Subira ya kuku na wanawe

**Na Adam Fungamwango**

KUNA methali kadhaa za kiswahili zimetengenezwa au kutungwa kimakakati sana na wahenga. Wanapotaka mtu awe na subira wanasema 'subira yavuta kheri.' Lakini wanapoona ni jambo ambalo linahitajika lifanyike kwa haraka, wanaigeuza na kusema 'ngoja ngoja yaumiza matumbo.'

Sasa hapo inategemea ni kitu gani kinatakikana ili methali moja itumike. Unahitajika uvumilivu, au jambo hilo linahitajika lifanyike haraka.

Mfano tuangalie filamu hii ya 'Ombi Langu' ndiyo tutaelewana.

Kijana mdogo anatokea kumpenda Hajra, lakini msichana huyo anaonekana kama vile hamuelewi. Kidogo anamwambia nia yake ni kutaka kumuoa, lakini anamwambie avute subira atamfikiria.

Siku zinapita, Lukuwi anamfuata nyumbani kwao kwenda kumuulizia tena, Hajra anamwambia aendelee kuwa mvumilivu,  lazima awe na subira na asiwe anamfuata sana nyumbani kwa shangazi yake anapoishi.

Masiku yanaenda, miezi na miezi lakini kimya, Lukuwi anamtafuta shoga yake Hajra na kumtuma kwenda kwao kuulizia, lakini anajibiwa maneno yale yale kuwa avumilie tu.

Jibu linarudishwa kwa Lukuwi, lakini linaonekana kuwa haridhiki. Lukuwi naamini kama kuna kitu ndani yake kwani kila siku amekuwa mtu wa kupewa ahadi tu.

Mwisho wa siku Hajra anakubali ombi la Hajra. Ni kama Lukuwi haamini hivi, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa binti amekubali.

Lukuwi anakwenda kumwambia mama yake. Mama anafurahi na kumwambia haraka atafute mshenga ili aoe haraka.

Mshenga anapeleka posa kwa shangazi yake. Lakini anaambia kuwa hawezi kuisoma peke yake kwa sababu yeye ni shangazi tu na wazazi wake wapo kijijini.

Taarifa inapelekwa kwa wazazi wake. Barua haiwezi kusomwa kabla wazazi hawajafika mjini, lakini nao wamekuwa wakipiga danadana licha ya kuambiwa kila kitu.

Wakaahidi watafika mjini, lakini terehe 21 walioahidi hawakufika.

Baada ya kutofika, Hajra anatoweka nyumbani, hajulikani alikokwenda. Siku tatu zinapita. Taarifa hizo zinapelekwa kwa wazazi wake kijijini kesho yake tu wakafika. Uchungu wa mwana ujuae mzazi.

haijulikani binti amekwenda wapi. Mzima au ameshakufa. Wakati wapo kwenye kikao. Lukuwi anaingia na Hajra. Wote wanashangaa. Lukuwi anasema yeye ndiye alimficha na kumhifadhi binti yao ili wazazi wake waje mjini. Anaomba msamaha kwa kufanya hivyo.

Mama yake Hajra anashinikiza barua isomwe haraka ili ndoa ifungwe lisijitokeze jambo lolote baya. Ndoa inafungwa.





# Akothee una mambo wewe

MSANII wa muziki na mjasiriamali, Esther Akoth, maarufu kama Akothee amedokeza kuwa mume wake Denis Schweizer anawakosesha wanaume usingizi kutokana na mambo adimu anayompatia.

"Siwezi kuolewa na mtu bila,chochote, ingalikuwa hivo ningekuwa niliolewa na hao kitambo,mimi ni mrembo na napendeza na ninavutia watu kama Omosh," alisema Akothee kupitia Instagram.

Akothee amesema mali si olote anafuata katika suala la kuolewa kwa sababu amejiendeleza na ana mali zake.



## Don Jazzy ulichokifanya kina thamani

MTAYARISHAJI maarufu wa muziki wa Nigeria, Don Jazzy, ametoa zawadi nono kwa mwanafunzi anayekabiliwa na changamoto shuleni.

Mwanafunzi huyo alituma ujumbe kwa bosi wa Mavin Records, akieleza jinsi shule ilivyokuwa ngumu na wanahisi kulemewa na changamoto zinazowakabili.

Akimjibu, Don Jazzy alionyesha kumuhurumia na kisha kumuuliza kama kiasi cha pesa ya nchi hiyo Naira 500,000 ingetosha kuwa kumbatio" la kweli kutoka kwake.


Aidha alimwagiza mwanafunzi huyo kumtumia maelezo ya akaunti yake ya benki iwapo watapata kiasi hicho kinakubalika.

## Bukunmi busara zako za kipekee

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Bukunmi Oluwasina ametoa onyo kali kwa wanaume akiwataka kutowataliki wake zao haraka kwa kosa la kukosa uaminifu.

Katika video iliyochapishwa kwenye ukurasa wake wa Instagram, Oluwasina aliwashauri wanaume haswa wale wa tasnia ya burudani, ambao visa vya talaka vimeongezeka maradufu.

Oluwasina alisisitiza kuwa badala ya kuendekeza talaka, wanapaswa kuwaombea wake zao ambao huenda hawakuwa waaminifu kutokana na shetani.





## Waliotaka kumteka Savage mbaroni

JESHI la Polisi la Nigeria, limesema limewakamata baadhi ya watu wanaotuhumiwa kufanya jaribio la kumteka nyara mwanamuziki, Tiwa Savage.

Msemaji wa idara uchunguzi makosa ya jinai, CSP Oluniyi Ogundeyi, alithibitisha kuwashikilia watu hao katika kituo kikuu cha Lagos.

Shirika la habari nchini humo (NAN) limeripoti kuwa habari za jaribio la kumteka nyara mwanamuziki huyo zilizuka Ijumaa kupitia mitandao ya kijamii.

## Sikienii Portable kafanya kweli

MWIMBAJI maarufu wa muziki wa hiphop ya mitaani, Portable, ametoa majibu ya kushangaza kwa wabaya wake, baada ya kufanya kufuru katika sherehe ya kuzaliwa ya mpenzi wake.

Tukio hilo ambalo lilikuwa la kifahari, lenye maonyesho ya kupindukia ya kimahaba ikiwamo kutia ndani shada la pesa, nguo zinazolingana za Ankara, bendi ya muziki na kofia zenye maandishi maridadi.

Sherehe hiyo ilifanyika katika baa yake katika Jimbo la Ogun, ambako watu walikusanyika kushuhudia sherehe hiyo ya kipekee.







Meneja wa wakala wa maji na usafi wa mazingira vijijini (RUWASA), Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, Mhandisi Joanes Martin (kulia), akisoma taarifa ya mkaguzi wa ndani ya kuanzia mwezi Juni na taarifa ya CAG mwaka 2021/2022 wakati wa mkutano wa nusu mwaka wa watumia maji, katika mji mdogo wa Orkesumet juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# RC aagiza kufuatiliwa nyumba zinazohamasisha ushoga

MKUU wa Mkoa Arusha, John Mongella, ameagiza vyombo vya ulinzi na usalama kufuatilia madai ya kuwapo kwa baadhi ya taasisi na nyumba za kifahari mkoani humo ambazo zinajishughulisha na masuala ya ushonga ili hatua kali za kisheria zichukuliwe dhidi yao.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha wakati akizindua vyumba vya madarasa manne yaliyogharimu Sh.milioni 80, kueleza kwamba hatakubali kuona taasisi au mtu anajihusisha na masuala hayo mkoani Arusha.

"Tunazo taarifa za kuwapo kwa baadhi ya taasisi na nyumba za kifahari ambazo zinakuta ndefu na mageti ya kifahari kumbe ndani yanaendelea masuala ya ushoga, tupo tunazifuatilia na nimeshaagiza viongozi wenzangu kufuatilia na hatutamuonea mtu ila atakayebainika katika hili tutamshughulikia,"alisema.

"Tamaduni hizi za ulawiti na ushoga tulizoletewa ziharibu taifa, hatuwezi kukubali kuziacha ziendelee kushamiri, ndugu zangu hali ni mbaya na nashukuru viongozi wa dini wanakemea hili bila ya kupepesa macho, hivyo wote tuungane kupinga.

"Arusha akitokea mtu au taasisi inashabikia ushoga hatutamuacha salama kama unataka jifungie chumbani kwako endelea, lakini ukitoka nje tuna wewe, lazima tutakukamata, hatuwezi kukubali kuvurugwa," alisema Mongella.

Kdhalika alitoa wito kwa watoto wa kike na kiume kutokubali mtu yeyote hata akiwa mwalimu wake kumpapasa mwilini, kwamba akikutana na hali hiyo watoe taarifa kwa viongozi au Jeshi la Polisi.

Alisema tatizo la ushoga linatengenezwa na watu wasioitakia mema Tanzania, hivyo kila mmoja kwa nafasi yake anapaswa kulikemea kwa nguvu zote.

Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtehengerwa, alisema hali ni mbaya kutokana na kukithiri kwa kesi za ulawiti na ushoga, hivyo vyema walimu wasaidie kushughulikia tatizo hilo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha, Steven Zelothe, aliwahimiza wanafunzi na walimu kushirikiana kukataa ushoga na wakisikia minong'ono au kuona dalili za watu kujihusisha na hilo wafichue kwenye vyombo vya dola.

# Maofisa watendaji H/shauri Arusha wakabidhiwa pikipiki

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MAOFISA watendaji kutoka kata nane za Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru mkoani Arusha, wamekabidhiwa pikipiki kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa wananchi wa eneo hilo.

Maofisa watendaji waliopatiwa pikipiki hizo ni kutoka kata za pembezoni za Bwawani Oljoro, Laroi, Musa, Oldonyowas, Oldonyosambu Lemanyata na Sambasha.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi pikipiki hizo, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Arusha, Seleman Msumi, alisema pikipiki hizo zitakuwa muhimu kwa watumishi hao wa serikali kwa kuwa zitasaidia kwenda kumaliza tatizo la kutembea umbali mrefu kwa watendaji.

Alisema kata hizo nane ziko maeneo ya pembezoni na kwa sehemu kubwa ya maeneo ya kiutendaji maofisa hao hulazimika kutembea umbali mrefu kuwafikia wananchi ili kuwapatia huduma.

Hata hivyo aliwataka kutumia pikipiki hizo kwa ajili ya kazi iliyokusudiwa na serikali ya kuwahudumia wananchi na siyo vinginevyo, huku akiwasisitiza kuzitunza na kuzithamini kwa kutambua kuwa ni mali ya umma.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arumeru, Noel Severe, aliipongeza serikali kwa kuteketeleza Ilani ya chama hicho kwa vitendo kwa kuhakikisha watumishi wanapata vitendea kazi vitakavyorahisisha utoaji na upatikanaji wa huduma kwa wananchi katika maeneo yao.

Aidha, watendaji hao waliipongeza serikali kwa kutambua umuhimu wa kuwapatia usafiri kwa kuwa awali tatizo la kukosa chombo cha usafiri kwenye maeneo yao liliwasumbua na kukwambia baadhi ya shughuli zao.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Oldonyosambu, Lomnyaki Ndiyogi, licha ya kuipongeza serikali alisema watumishi hao walikuwa wakitembea kilomita 50 na walitumia zaidi ya saa nane kufanya kazi moja.

Alisema: "Kupitia pikipiki hizi zinakwenda kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wetu, kwa kuwa awali tulikuwa tunafanya kazi kwa siku nzima na sasa tunahakika kwa kupatiwa vyombo vya usafiri tutatumia saa moja, tunaishukuru serikali na tunaahidi kuwahudumia wananchi kwa kasi kubwa".

# Kifungo cha miaka 30 kwa kumbaka 'house girl'

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara, imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela mkazi wa Kijiji cha Gendi, Issaya Mtinangi (35), kwa kosa la kumbaka mfanyakazi wa ndani (15) (jina limehifadhiwa).

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario.

Akisoma hukumu hiyo, alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo Desemba 15 mwaka jana majira ya mchana katika Kijiji cha Gendi kwa kufanya mapenzi na binti wa miaka 15 bila ridhaa yake.

Alisema shahidi namba moja ambaye ndiye mwathirika alidai mahakamani hapo kuwa Mtinangi ndiye aliyemtafutia kazi za ndani. Alisema mshtakiwa alimtoa binti huyo Kateshi akiwa na mwenzake na aliwapeleka jirani na ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na baada ya kuwafikisha eneo hilo binti huyo alimpeleka hadi mtaa wa Ngarenaro ulioko Babati Mjini na kumkabidhi kwa mama Amina kwa ajili ya kufanya kazi za ndani.

Alisema mshtakiwa alikiuka kifungu cha 130(1)(2)(e) na kifungu cha 131(1) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kama iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Aidha, alisema siku ya tukio mshtakiwa aliienda kwenye familia ya binti huyo alipokuwa anafanya kazi na kuwaambia kuna ndugu zake wanamhitaji wakamuone, kwamba alimpeleka nyumbani kwake Gendi na kumlazimisha kufanya mapenzi.

Kimario alisema shahidi huyo alidai mahakamani kuwa alimuingilia mara mbili na baada ya kitendo hicho alimwamuru kupika ugali na wakati akipika mshtakiwa alipitiwa na usingizi na binti huyo alipata nafasi ya kukimbia.

Alisema binti huyo alipiga kelele za kuomba msaada, alisaidiwa na wasamaria wema na kwenda kituo cha polisi.

Alisema Mahakama imemtia hatiani mshtakiwa baada ya upande wa mashtaka kupeleka mashahidi wanne ambao walitoa ushahidi usioacha shaka na mshtakiwa alijitetea mwenyewe.

Vilevile alisema kwa mujibu wa vipimo vya daktari vilimeonyesha kuwa binti huyo alibakwa baada ya kukutwa na mbegu za kiume. Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Emmanuel Jumbe, kabla ya kutolewa hukumu hiyo alida mshtakiwa huyo hana kumbukumbu za kutenda makosa ya jinai, hivyo Mahakama itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa jamii.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea aliiomba Mahakama hiyo imwangalie kwa jicho la huruma kwa kuwa mama yake amezeeka na anamtegemea pia anaalea mtoto wa dada yake ambaye alishafariki dunia.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kutoka 'taipuraita', kompyuta ya chogo hadi 'flati leo hii

**Na Adam Fungamwango**

DUNIA inakwenda kasi sana, miaka ya 1970, 1980, hadi 1990 kwenye maofisi kulikuwa na mashine ya kuchapa maneno iliyoitwa 'typewriter' kwa lugha ya kingereza, na neno ambalo limetoholewa kwenye lugha ya kiswahili ikaitwa 'taipuraita.'

Miaka hiyo ilikuwa ni kifaa au mashine iliyokuwa kwenye wakati, kwani kilionekana kuwa na kasi kuliko kuandika kwa mkono.

Na siyo kila mmoja alikuwa anaweza kukitumia, badala yake kulikuwa na watu waliokuwa wanaitwa masekretari, au makatibu muhtasi ambao moja kati ya kazi zao zilikuwa ni kuchukua barua zilizoandikwa na mabosi kwa mkono, au kutoka nje ofisi na wao wanazichapisha kwenye mashine hizo kwa sababu za kiofisi.

Kama ni barua sasa ilikuwa inaonekana vema na kuvutia hata machoni kuiona na kuisoma tofauti na mwanzo ilivyoandikwa kwa mkono.

Makampuni, mashirikia na maofisi yote ya serikali na hata baadhi ya mahakama zilikuwa na 'taipureta' ili ilionekana ya kisasa ni lazima uwe nayo.

Hata baadhi ya makampuni ya magazeti yalitumia 'taipuraita' kwenye kazi zao na waandishi wa habari walitakiwa kujifunza ili kurahisisha kazi, badala ya kuandika na mkono kwenye karatasi.

Kwa wakati huo ilikuwa ndiyo teknolojia mpya na ilionekana inafanya kazi kwa haraka. Na kweli



ilikuwa hivyo kwani haikuwa sawa na mtu anayeandika kwa mkono.

Ni kama simu vile, zamani hakukuwa na simu za mkononi, bali za mezani na asilimia zaidi ya 90 zilikuwa maofisini.

Matra nyingi wanaokuwa rahisi kupatikana kwenye mawasiliano ni wale ambao wameajiriwa kwenye mashirika, makampuni na maofisini.

Mtu atatafuta simu ya mkononi popote pale na kumpigia anayemtaka. Simu itapokelewa na mtu anayeitwa opereta ambaye naye ndiyo atafanya kazi ya kuiunganisha kwenye idara ambayo mlengwa anafanyia kazi.

Wakati huo aliyepiga simu ameshaambiwa asubiri, na atafanya hivyo kiasi cha dakika tano mpaka 10, ndiyo ataambia aongee kwa mlengwa.

Unaweza kuona ni kama stori za kufikirika, lakini ndiyo ukweli. Hadi leo hii unapiga tu namba inakwenda moja kwa moja kwa mlengwa, kazi kubwa imefanyika na hii ndiyo maana ya ule msemo wa dunia inakwenda kasi sana.

Siku hazigandi, Tanzania ikapata ugeni wa kitu kinachoitwa kompyuta.

Ni kitu ambacho kilikuwa kigeni kiasi kwamba wengi walishindwa kutofautisha kati ya kompyuta na televisheni.

Kwa sababu zote zilizoingia wakati huo zilikuwa za 'chogo'. Nilisema chogo ndiyo naelekweka vizuri zaidi kwani ni msamiati ambao unaeleweka kwa urahisi zaidi.

Televisheni na kompyuta zilizoingia miaka hiyo ya mwanzo wa 1990, zilikuwa na muundo kama boksi au sanduku hivi, na kadri teknolojia ilivyozidi kukua, watoto wa mjini wakawa wanatoa majina ya vile vitu vilivyoonekana kupitwa na wakati.

Kompyuta hizo zilingia na kusababisha 'taipureta' kuonekana haina maana tena. Kwenye makapuni, mashirika au ofisi mtu akikutana na 'taipureta' anashangaa na wafanyakazi wa hapo wamepitwa na wakati.

Makampuni ya magazeti na redio nayo yakaanza taratibu kuachana na 'taipureta' na kununua kompyuta hizo ambazo kwa wakati huo zilionekana za kisasa mno kutokana na teknolojia ya wakati huo.

Kompyuta hizo zilitamba sana hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000, zikaanza kuingia aina nyingine za kompyuta ambazo hazikuwa kwenye muundo wa sanduku au chogo. Hizo ziliitwa 'flati.'

Yaani kama vile televisheni za chongo zilivyoanza kupitwa na wakati na kuja za 'flati', hata kompyuta nazo ikawa hivyo hivyo.

Kama kawaida, kwenye makampuni mbalimbali yakiwemo ya habari, na mengine wakaanza kununua aina hizo za kompyuta na kuachana na za chogo, kiasi kwamba ikionekana inakuwa ni aibu.

Kwa bahati nzuri zaidi ni kwamba televisheni za 'flati' zilizoingia hivi sasa zimekuja pamoja na mabadiliko mbalimbali makubwa ya teknolojia ikiwemo 'intateti', na vifaa vingine mbalimbali vya ziada na mifumo ya kurahisisha zaidi mawasiliano tofauti na ile ya zamani.





# Sudan bado hali tete; 20,000 wakimbilia Chad

**KARTOUM,** SUDAN

SHINIKIZO kubwa la kidiplomasia linaongezeka kutaka kusitishwa mapigano yanayoendelea nchini Sudan.

Mpaka jana kumeripotiwa vifo vya zaidi ya watu 300 tangu mapigano hayo yaibuke wiki iliyopita.

Jeshi la Sudan limekuwa likipambana na wanamgambo wanaoitwa Rapid Support Forces (RSF).

Umoja wa Mataifa, Marekani na mataifa mengine yametoa shinikizo la kusitishwa kwa vita kwa muda wa siku tatu kuadhimisha sikukuu ya waislamu ya Eid el-Fitr.

Hata hivyo RSF ilisema imekubali kusitisha mapigano ya saa 72 kwa misingi ya kibinadamu.

Hakukuwa na kauli kutoka kwenye jeshi la nchi hiyo.

Taarifa ya wanamgambo hao ilisema, usitishaji vita utakuwepo kuanzia saa 06:00 ya jana ili iendane na sikukuu.

Majaribio mawili ya awali ya kusitisha mapigano yalishindwa kutekelezwa.

Mkuu wa Jeshi, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, awali alipuuza uwezekano wa mazungumzo na RSF.

Matumaini ya kupatikana kwa mapatano ya muda yalikuja baada ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres kutoa wito wa kusitishwa kwa mapigano ili kuruhusu raia kupata usalama.

Alisema usitishaji vita kwa ajili ya Eid lazima iwe hatua ya kwanza katika kutoa ahueni ya mapigano na kuandaa njia ya usitishaji mapigano wa kudumu.

"Usitishaji huu wa mapigano ni muhimu kabisa kwa sasa," alisema Guterres

Umoja wa Mataifa umeonya kuwa kati ya watu 10,000 hadi 20,000, wengi wao wakiwa wanawake na watoto wamekimbia kutoka Sudan kutokana na mapigano makali na kwenda nchi jirani ya Chad.

Hata hivyo, jana kulikuwepo na mapigano ya hapa na pale katika mji mkuu wa Sudan Khartoum, licha ya kikundi cha kijeshi cha Rapid Support Forces (RSF) kusitisha mapigano.

Umoja wa Mataifa na nchi kadhaa zinaendelea kuzishawishi pande mbili kukubali mkataba wa usitishaji mapigano.

Kikundi cha RSF kilisema kimelazimishwa kuchukua hatua ya kujilinda ili kuzuia kile kilichoita jaribio la mapinduzi, lakini kitaheshimu mkataba.

Mkuu wa majeshi, Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, hakutaja lolote kuhusiana na usitishaji wa mapigano katika hotuba yake iliyorekodiwa kwenye mtandao wa kijeshi wa Facebook.

Alisema kwamba bado anajitolea kurejesha utawala wa kiraia nchini Sudan, na akatoa wito kwa kila mtu kuheshimu kauli mbiu inayosema jeshi moja, watu wamoja.

Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) limesema limesikitishwa na kuongezeka kwa ghasia nchini Sudan na kusababisha wimbi la watu kuwasili nchini Chad.

"Mahitaji muhimu zaidi ni maji, chakula, malazi, huduma za afya, ulinzi wa watoto na kuzuia unyanyasaji wa kijinsia," taarifa ya shirika hilo iliongeza.

**BBC**



Chombo cha anga za juu cha kizazi kijacho cha SpaceX cha Starship, kikiwa katika roketi yake yenye nguvu kwa ajili ya kurushwa anga za juu. Hata hivyo chombo hicho kililipuka baada ya kuruka karibu na Brownsville, Texas, nchini Marekani juzi. **PICHA: REUTERS.**

# Ethiopia yakana kushambulia mpaka

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

WAZIRI Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, amekanusha ripoti kuwa jeshi la Ethiopia lilishambulia vikosi vya Sudan katika eneo la mpakani.

Aidha, amewaonya wanaoeneza taarifa hizo kuacha, kwani hakuna faida ya kisiasa wanayoweza kuipata.

"Baadhi ya watu walikuwa wakisambaza madai ya uongo ili kufanikiwa kisiasa wakati ambao watu wa Ethiopia na Sudan wanakabiliwa na changamoto nyingi". Alisema Abiy.

Akitumia ukurasa wake wa Twitter, Abiy, aliongeza "Tunalaani vikali madai hayo ambayo yanalenga kuharibu uhusiano wetu wa kindugu na ujirani kati ya Ethiopia na Sudan,"

Kauli ya kiongozi huyo yanafuatia ripoti kwamba vikosi vya Ethiopia vilishambulia wanajeshi wa Sudan katika eneo linalozozaniwa la al-Fashaga, siku ya Jumanne, huku kukiwa na mapigano yanaendelea kati ya vikosi hasimu nchini humo.

Sudan na Ethiopia zimekuwa katika mgogoro kuhusu eneo la al-Fashaga, huku Sudan ilituma wanajeshi huko na kuchukua udhibiti wa sehemu kubwa ya eneo hilo mnamo 2021.

**BBC**

# Marekani kuendesha mafunzo ya vifaru wanajeshi Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

JUMLA ya vifaru 31 aina ya Abrams vitawasili katika uwanja wa mazoezi ya kijeshi wa Grafenwoehr nchini Ujerumani mwishoni mwa mwezi Mei, kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wanajeshi wa Ukraine.

Taarifa hiyo imetolewa wiki kadhaa baada ya jeshi la Ukraine kutangaza litaanza kufunzwa jinsi ya kuvitumia vifaru hivyo kwa wiki 10.

Shirika hilo pia lilisema katika taarifa yake kwamba wanajeshi wapatao 250 wa Ukraine watapewa mafunzo, ambapo baadhi yao watajifunza jinsi ya kutumia vifaru hivyo, huku wengine wakijifunza kuviukarabati na utunzaji wake.

Uamuzi wa marekani wa kutuma makombora 31 ya Abrams nchini Ukrainem uliochukuliwa ni kinyume na msimamo wa awali wa nchi hiyo, ambayo awali ilisema kwamba vifaru vya Abrahams ni vigumu kutumiwa na ni ghali kuviendesha.

Tangu mwanzoni mwa vita, jeshi la Marekani limewapatia mafunzo wanajeshi zaidi ya 7,000 wa Ukraine kuhusu jinsi ya kutumia aina nyingine za silaha.

**BBC**

# Msaidizi wa rais Mali auawa

**BAMAKO,** MALI

MKUU wa utumishi wa kiongozi wa kijeshi nchini Mali, ni miongoni mwa watu wanne waliouawa katika shambulizi la jana.

Oumar Traore, ambaye ni mkuu wa utumishi wa Kanali Assimi Goita, aliuawa katika shambulizi lililofanywa kaskazini mwa mji mkuu Bamako, karibu na mpaka wa Mauritania.

Taarifa kutoka ofisi ya rais ilisema mazishi yangeanyika kana katika mji ulio na kambi ya kijeshi wa Kati, karibu na mji mkuu Bamako.

Hakuna yeyote aliyedai kuhusika na shambulizi hilo.

Mali imekuwa ikikabiliwa na mgogoro wa kiusalama na kisiasa tangu uasi wa itikadi kali na makundi yanayotaka kujitenga ulipozuka kaskazini mwa nchi hiyo mwaka wa 2012.

Tangu 2020 imekuwa chini ya utawala wa kijeshi unaoongozwa sasa na Kanali Assim Goita.

**DW**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROSS HAMISI BEHEWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI JIMNY yenye usajili namba T 271 DLY, CHASSIS NAMBA: JB23W216759 na ENGINE NAMBA: K6AEAA901685. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/138743/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NECHI JOHN LYAMUYA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA NOAH yenye jina la umiliki BONSTAR BUILDING MATERIAL CO. LTD yenye usajili namba: T 216 DHJ, CHASSIS NAMBA: AZR603083827 na ENGINE NAMBA: 1AZ5531229. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.


**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/138594/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TABU MASOUD SEFU,** Anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye INDEX NO S0744-0071 kilichotolewa na BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA kupitia shule ya Sekondary NANGA Mwaka 2015 Yeyote akaekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.

**TAARIFA YA POLISI: MAS/RB/339/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMMANUEL SIMON OMARY** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index No. S2697-0049 kilichotolewa na Baraza la Mitihani Mwaka 2019 Shule ya Sekondari IPARAMASA. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Taarifa polisi: DOD/DOD/RB/134509/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA63)**
**Mahakama ya Mwanzo**
**Wilaya ya Karagwe**
**MADAI YA TALAKA NO 05/2023**
**Mdai DIANA MWESIGWA**
**Mdaiwa DEOGRATIAS NICOLAUS KIDENKE**
**KWA DEOGRATIASNICOLAUS KIDENKE**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai ya talaka kwamba ANAKUDAI TALAKA**

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hiisiku ya tarehe 28/04/2023 saa 2:00 Asubuhi kwa kujibu Madai hayo.Na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta Mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu,Mahakama ikithibitisha kama umepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 18/4/2023

**Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo**
RESIDENT MAGISTRATE NYABIYONZA PR. COURT KARAGWE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MBEYA**

**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 61/2022**
**(Asilia Shauri la Jinai Na. 158/2021, Mahakama ya Wilaya Chunya)**
**JAMHURI..............................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**OBED MWANIJEMBE LAZARO...............MJIBU RUFAA**

KWA BWANA: **OBED MWANIJEMBE LAZARO**
**POPOTE ULIPO TANZANIA**

### KUITWA SHAURINI

Unaamuliwa na Mahakama hii, kuhudhuria hapa Mahakamani tarehe **02/05/2023** siku ya Jumatatu saa **3.00** asubuhi bila kukosa.

**ELEWA KWAMBA,** ukikosa kufika Mahakamani siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe **21/11/2022**

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 40 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late MELEA MBILYO MTUZA**
**Of Chamwino within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY ALFA GILBERT MTUZA**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 24 Day of 4, 2023

Date at Dodoma this 3rd day of April, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 36 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**THEOBARD PETRO NYAGALI**
**Of Chidachi within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY SELINA PETRO MAGOME**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 24th Day of APRIL, 2023

Date at Dodoma this 22nd day of MARCH, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.39 OF 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**PAULO PATRICK MALINGUMU**
**Of Bihawana within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY STELLA PAULO MALUNGUMU**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 24TH Day of APRIL, 2023

Date at Dodoma this 5thday of April, 2023

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GABRIEL JOHN MIHAMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA PORTE yenye usajili nambaL: T212 CD99 iliyotolewa na TRA. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chocote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: + DAR/OST/RB/13846/2023**


# OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
Website: www.ippmedia.com


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumbani moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-5

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Sajenti Mosses aliridhika na majibu ya mama Miraji pamoja na Bi Mkali, akawaaga na kuahidi kama kutakuwa na kitu cha ziada basi angerejea tena. Wakamuaga kwa bashasha kwa sababu hawakuona dalili yoyote ya wao kuhisiwa au kuambiwa kitu chochote kwamba kuna kitu walikosea kwenye tukio zima.

Kwa jinsi upelelezi wa muda mfupi tu ambayo ameufanya, aliona kabisa kuwa wazoa taka ambao huwa wanapenda kutembea alfajiri kwa ajili ya kutelekeza viroba vya taka kwenye vichochoro vya nyumba za watu, au waokota chupa za plastiki ambao nao wana tabia ya kuamka alfajiri kwa ajili ya kuwahi chupa zilizotupwa usiku na watumiaji kwa ajili ya kwenda kuziua, ndiyo waliohusika na tukio hili na si vinginevyo. Tayari alishatoa amri ya kukamatwa, kilichobaki ni kuwahoji ili kumpata muuaji.

*********************************




Aliwaangalia askari wenzake kwa zamu akiwa anachezesha kalamu yake mezani kukiwa na karatasi.

"Kazi bado ni ngumu." Akaambia wenzake kwa namna kuonyesha uhalisia wa jambo.

"Nimechukua ripoti zetu wote wawili, pamoja yale niliyoagiza, inaonekana bado hatujapiga hatua hata moja kwenda mbele kuhusiana na kuuawa kwa Tessy."

"Kwa vipi Inspekta?" Sajenti Moses alijikakamua kumuuliza bosi wake.

"Ni kweli kila mmoja nilimpa kazi ya kwenda kuwahoji waliokuwepo eneo la tukio, lakini pia tuliwakamata vijana waokota chupa za plastiki na wazoa taka, lakini kwa jinsi kazi ilivyofanyika bado sana."

"Ina maana mpaka sasa hakuna japo fununu?"

"Ni hivi, tuliwakatama vijana 35, na kati yao, watano wamekiri kuwa wamehusika kwenye mauaji." Inspekta Frank alinyamaza na kuwazama wenzake.

"Sasa kama wamekiri kazi inakuwa ngumu kivipi afande?" Kwa mara ya kwanza koplo Ben akauliza.

"Hapo hakuna usawa wowote afande Ben. Haiwezekani watu watano wote wakiri kufanya mauaji ya mtu mmoja."

"Siyo kwamba wameshirikiana?"

> **"Tupate mtu mmoja mtaalam wa masuala ya upelelezi ili atusaidie kwenye hili."**

"Hapana. Kilichofanyika ni kufanya nao mahojiano kila mmoja peke yake. Kwanza walikataa. Lakini ilipotumika nguvu kidogo, baadhi wakakubali. Na kila mmoja akakubali kivyake kuwa ni kweli ameua. Kila mmoja akakiri ameua peke yake."

Sajenti Moses na kople Ben walimtazama bosi yao na kweli ikawaingia akilini kuwa haiwezekani watu watano kila mmoja akakiri kumuua mwanamke huyo huyo mmoja, kila mmoja akisema amefanya mauaji hayo peke yake.

"Hii inaonyesha kuwa watu wetu waliotumia nguvu kidogo wamesababisha baadhi wakikiri kuwa amefanya kitendo hicho lakini si kweli. Maiti mmoja kwa wauaji watano si kweli."

"Afande, mimi nadhani labda hao 30 waliobaki waachie, na watano waliobaki uanze tena mchujo, tunaweza kupata mmoja ambaye amefanya tukio hilo." Akashauri afande Moses.

"Ni kweli tutafanya hivyo, lakini mimi bifasi nadhani kuwa hawa walikubali ili kuepuka kibano kikali walichokuwa wakikipata, lakini hatujakata tamaa, tutaendelea na upelelezi wetu." Inspekta Frank akaahidi.

"Hawa waliobaki?" afande Ben akauliza.

"Wiki ijayo tutawapeleka mahakamani, halafu wataachiwa kwa dhamana, watarudi uraiani kuendelea na shughuli zao za kawaida, chochote au yoyote atakayehitajika baadaye tutamfuata." Akamaliza inspekta Frank, lakini kama kuna kitu akakumbuka. "Hebu subirini kwanza." Moses na Ben wakapiga saluti na kukaa tena kwenye viti.

"Nimewaza na kuwazua, nimeona kama tukishindwa kupata fununu ya chochote baada ya mchujo huu wa watu watano, nitakazimika kuomba nguvu mahala."

"Nguvu gani afande?" Afande Moses akauliza.

"Tupate mtu mmoja mtaalam wa masuala ya upelelezi ili atusaidie kwenye hili."

"Ina maana sisi hatuwezi kuendelea na upelelezi huu?" Akauliza tena.

"Tunaweza, lakini ama tunaweza kuchukua muda mrefu sana, au tusimpate kabisa muuaji. Kama hakupatikana kwa hawa waokota makopo na wazoa taka, basi inabidi kazi ya ziada ifanyike.

Kama siyo hawa, basi muuaji atakuwa mtu ambaye anayeifahamu kazi yake vema, ambaye atakuwa amefanya hivi kwa makusudi kutengeneza mazingira ya kutuaminisha sisi askari polisi kuwa hawa vijana ndiyo wamefanya mauaji haya."

Kwa mara ya kwanza Moses na Ben, wakatikisa kichwa kwa pamoja kukubaliana na anachoongea bosi wao.

"Tuombe Mungu tumpate kati yao, lakini tukimkosa, basi kazi hii itakuwa ngumu zaidi na itahitaji mtaalam zaidi."

"Kwa nini umefikiria hivyo afande?"

"Ni kwamba siyo kama sisi hatutoweza, ila muda unaweza kuwa mrefu mno, na pia tunaweza kuumiza watu wengi ambao hawahusiki.

Hivi afande Moses, naweza hapa kukutuma kwenda kumkamata yule mama Miraji na mumewe kuwa wanahusika unaweza kukubali hilo? Kukubali unaweza kukubali kwa sababu ni amri ya mkubwa wako, je unaweza kuamini?" Swali hilo nusura limchekeshe afande Moses.

Akamkumbuka mama Miraji, mwanamke mcheshi matata ambaye alikutana naye na kumhoji, akifuatiliwa kesi huu.

"Kwangu mimi afande sidhani."

"Kwa nini?"Akauliza inspekta Frank.

"Kwanza haiwezekani mtu na mumewe wote wamuue mtu mmoja, tena mwanamke. Halafu siyo kumuua tu, wamkatekate viungo, mmh, hapana."Inspekta Frank akaangua kicheko.

"Ndiyo maana nimeona hapa tunapoendea kila mmoja tutamuona anahusika na mauaji haya, hivyo tumuongeze mtu mmoja mwenye utaalam zaidi yenu nyinyi."

"Sawa, haina neno afande, atatoka hapa hapa kwenye Jeshi la Polisi?"

"Kwetu sisi hapa nyinyi peke yenu wawili mnatosha. Nchi hii ina idara nyingi za kuilinda nchi na wananchi wake, hivyo wiki ijayo nitakuja kuwatangazia ni nani nimemuongeza na ametoka wapi. Nadhani hiyo inaweza kutusaidia kwenye hili kwa sababu wananchi kila kukicha wamekuwa wakifuatilia vyombo vya habari kutaka kujua tumefikia wapi kwenye tukio lile baya la mauaji ya binti yule, Tessy."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# RUVU VS AZAM KAZI IPO LEO

**Shufaa Lyimo na Hadija Mngwai**

TIMU ya Azam FC imejiandaa kuhakikisha inaondoka na pointi zote tatu kwenye mchezo wao wa leo wa Ligi Kuu Tanzania bara dhidi ya Ruvu Shooting, huku wapinzani wao wakipania kupambana kutoshuka daraja.

**Kocha msaidizi wa Azam, Agrey Moris alisema amekiandaa vema kikosi hicho kwa ajili ya ushindi kwenye mchezo huo ambao wao watakuwa ugenini.**

"Tutaingia kwenye mchezo huu tukiwa na lengo moja tu la kuhakikisha tunavuna pointi zote tatu, tunaomba mashabiki wetu waendelee kutupa ushirikiano," alisema Moris.

Alisema kila mchezaji ana morali ya juu kuhakikisha anaipa ushindi timu yake.

Alisema msimu huu umekuwa na ushindani mkubwa kwani kila timu imejipanga vizuri ikiwa ni pamoja na kufanya maandalizi ya muda mrefu ili isishuke daraja.

"Mchezo unatarajiwa kuwa mgumu na wenye upinzani kutokana na ubora wa timu zote mbili, tunamheshimu mpinzani wetu na tunafahamu timu hiyo ina wachezaji wazuri, hivyo sisi tumejiandaa kuhakikisha tunaondoka na pointi tatu," alisema.

Kwa upande wake Ruvu imetangaza vita kwa mechi nne zilizobakia za Ligi Kuu Bara kuhakikisha inajinasua katika hatari ya kushuka daraja na itapambana kuhakikisha inashinda zote ili iweze kujikusanyia pointi 12 zitakazowaweka sehemu salama.

Ruvu ipo nafasi ya 15 ya msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 20 na ipo kwenye hatari ya kushuka daraja.

Ofisa Habari wa Ruvu Shooting, Masau Bwire amesema kuwa, lengo lao moja kubwa ni kuhakikisha wanaibakisha timu Ligi Kuu msimu ujao kupambana katika mechi nne zilizobakia.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunapata ushindi ili kuweza kuinusuru timu kushuka daraja na kuhakikisha inabaki Ligi Kuu kwa kufanya vizuri katika mechi zilizobakia.

"Maana tukifanya vibaya kwa kutoshinda ni wazi tunashuka daraja jambo ambalo hatulihitaji litokee, lakini tuna imani kubwa ya kuweza kubaki Ligi Kuu msimu ujao, na mwalimu anakiandaa vyema kikosi kuelekea mechi nne za mwisho ambazo tumepanga kushinda," alisema Bwire.

Aidha aliongeza kuwa, "Tuna majeruhi mmoja tu ambaye ni Abdullahman Mussa ambaye alivunjika mguu katika mchezo wetu wa kirafiki tuliyocheza na Mbeya City hivi karibuni, hivyo atakosa michezo iliyobakia."



Mcheza Tenis, Paul Malya akipiga mpira kurudisha kwa mpinzani wake hayupo pichani wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Kijitonyama jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# *Nane bora Daraja la Pili kuanza Jumatatu*

**Na Adam Fungamwango**

HATUA ya nane bora Ligi Daraja la Pili 'first league' inatarajia kuanza kutimua vumbi Jumatatu ya Aprili 24 hadi Mei 2 mwaka huu kwenye Uwanja Azam Complex, Chamazi, kusaka timu tatu zitakazopanda, Ligi ya Championship kuchukua nafasi ya zitakazoshuka.

Taarifa iliyotolewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), timu zilizofanikiwa kuingia hatua hiyo kutoka kwenye makundi manne, ambapo kila kundi ilitoa timu mbili, African Lyon, Alliance FC, Dar City, Cosmopolitan, Lipuli FC, Rhino Rangers FC, Stand United na TMA.

Timu hizo zimepangwa kwenye makundi mawili, A na B, ambapo Stand United, Allinace FC, Cosmopolitan na Lipuli zipo kundi A na African Lyon, Rhino Rangers, TMA na Dar City zipo Kundi B.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolea na TFF, Stand United itafungua utepe kwa kucheza dhidi ya Alliance Aprili 22, ambapo baadaye Cosmo itakipiga dhidi ya Lipuli, huku Kundi B likianza kukipiga Aprili 23, African Lyon ikapocheza dhidi ya Rhino, na TMA itakipiga dhidi ya Dar City.

Nusu fainali zote mbili zinatarajiwa kuchezwa Mei Mosi na fainali itachezwa Mei 3 pamoja na kusaka mshindi wa tatu, ambapo timu zitakazocheza fainali zote zitakuwa zimeshapanda Ligi ya Championship, ambapo timu zitakazofungwa kwenye hatua ya nusu fainali nazo zitacheza mechi ya mchujo na mshindi ataungana na timu mbili zilizotinga fainali kupanda kwenye ligi hiyo.

## Fountain yajizogeza mbio za ubingwa Ligi Kuu Wanawake

**Na Kastuli Elias,** MWANZA

KOCHA wa timu ya Fountain Gate Princess, Juma Masoud amewapongeza wachezaji wake kwa kufuata vizuri kile alichowaelekeza baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Alliance Girls kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania bara, uliopigwa uwanja wa Nyamagana, jijini Mwanza juzi.

Mabao ya Fountain Gate kwenye mchezo huo yalifungwa na Privilege Mupeti na Frida Mbango 'Wonderkid', wakati lile la Alliance Girls likiwekwa kimiani na mshambuliaji wake, Winfrida Charles.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, kocha Masoud alisema kwamba, ameridhishwa na kiwango kilichooneshwa na timu yake na amefurahishwa na namna walivyoweza kufuata vizuri maelekezo yake.

"Nafurahi kwa matokeo haya na nawapongeza wachezaji wangu kwa kwa sababu kwa kiasi kikubwa walifuata maelekezo niliyowapa kabla ya mchezo huu na hatimaye tumeibuka na ushindi," alisema Masoud.

Aidha aliongeza kuwa ushindi huo umefufua matumaini ya timu yake katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake msimu huu.

"Ushindi huu ni mhimu kwetu kwa sababu unaenda kuongeza presha katika mbio za kuwania ubingwa na pia umeturudisha rasmi katika kuwania ubingwa huu msimu huu."

Kwa upande wake Kocha Mkuu wa Alliance Girls, Ezekiel Chobanka alisema malengo yake yapo palepale licha ya kupoteza mchezo huo.

"Nakubali nimepoteza mchezo wa leo (juzi) lakini malengo yangu ni kukusanya alama 26 na nina uhakika nitazipata katika michezo minne iliyobaki," alisema.

Kwa matokeo hayo sasa Fountain Gate wamefikisha alama 31 na wapo kwenye nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi ya Wanawake nyuma ya Simba Queens wenye alama 33 katika nafasi ya pili na JKT Tanzania wapo kileleni wakiwa na pointi 34 na Alliance wao wamebaki na alama zao 20 katika nafasi ya tano.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**POCHETTINO AWANIA CHELSEA**
KOHA wa zamani wa Paris St-Germain na Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino mwenye umri wa miaka 51 amefanya mazungumzo na Chelsea kuhusu kuinoa klabu hiyo ya London. (*Mirror*)

**NYOTA WENGI KUUZWA**
CHELSEA inapanga kuuza nyota wake wengi kabla ya Juni 30 ili kusalia ndani ya sheria za kifedha. (*Evening Standard*)

**DE GEA KUSAINI**
GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea mwenye umri wa miaka 32, yuko mbioni kusaini mkataba mpya wa kusalia katika klabu hiyo. (*Forbes*)

**HOJLUND ATAKIWA MAN**
MANCHESTER United inaongoza katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Atalanta na Denmark, Rasmus Hojlund mwenye umri wa miaka 20. (*Mirror*)

**MESSI KUREJESHWA**
KLABU ya Barcelona inakamilisha ofa ya kupeleka Paris St-Germain kwa ajili ya kumrejesha mshambuliaji wa Argentina mwenye umri wa miaka 35, Lionel Messi. (*Mundo Deportivo*)

**ROWE ATAKIWA VILLA**
KLABU ya Aston Villa imeibua tena nia yao ya kumnunua kiungo mshambuliaji wa Arsenal na England, Emile Smith Rowe mwenye umri wa miaka 22. (*talkSPORT*)

**TORRES MKATABA MPYA**
KLABU ya Villarreal inatazamiwa kumpa beki wa Hispania, Pau Torres mkataba mpya huku Aston Villa ikipanga kujaribu kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 msimu huu. (*Football Insider*)

**KOVACIC ATAKIWA CITY**
KLABU ya Manchester City inataka kumsajili kiungo wa kati wa Chelsea na Croatia, Mateo Kovacic mwenye umri wa miaka 28 katika dirisha lijalo la msimu huu wa joto licha ya pia kutaka kusalia katika mbio za kumnunua nyota wa Borussia Dortmund na England, Jude Bellingham mwenye umri wa miaka 19. (*Givemesport*)

**THURAM AWANIWA PSG**
KLABU ya Paris St-Germain huenda ikamsajili kiungo wa kati wa Nice na Ufaransa, Khephren Thuram mwenye umri wa miaka 22 au kiungo wa kati wa Lens na Ivory Coast, Seko Fofana mwenye umri wa miaka 27 kama mbadala wa Jude Bellingham. (*CaughtOffside*)

**SAINT-MAXIMIN KUUZWA**
KLABU ya Newcastle United iko tayari kumuuza winga Mfaransa mwenye umri wa miaka 26, Allan Saint-Maximin ili kupata fedha kwa ajili ya usajili katika dirisha lijalo la usajili. (*talkSPORT*)

**MAZRAOUI AFUATILIWA**
KLABU za Manchester United, Newcastle, Wolves, Arsenal, West Ham na Crystal Palace zote zinamfuatilia beki wa pembeni wa Morocco na Bayern Munich, Noussair Mazraoui mwenye umri wa miaka 25. (*90min*)

**SMALLING KUONGEZA**
MLINZI wa England, Chris Smalling mwenye umri wa miaka 33 yuko katika hatua ya mwisho ya mazungumzo na AS Roma ili kuongeza mkataba mpya kuendelea kusalia Italia hadi Juni 2025. (*Fabrizio Romano*)

## DONDOO ZA[...]KA MAGAZETI Y[...]YA



# TEN HAG AKOSOA UCHEZAJI WA MAN UTD

**Asema wachezaji walikuwa hawana utayari, hivyo wametolea Europa...**

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag ameikosoa Manchester United kwamba, haikuwa na "shauku, nia na utayari" baada ya kutolewa kwao kwenye robo fainali ya Ligi ya Europa mikononi mwa Sevilla, Alhamisi.

**United, ambao walijifunga wenyewe mabao mawili katika mechi ya mkondo wa kwanza wiki iliyopita na kutoka sare ya 2-2, walijikuta wakipoteza kwa uwiano wa mabao 5-2 pale kweye dimba la Roman Sanchez Pizjuan.**

Kwa mara nyingine, kikosi cha Ten Hag kiliipa Sevilla mabao mawili kwa Youssef En-Nesyri kufunga mara mbili akitumia makosa ya Harry Maguire na David de Gea.

United hawakuwa na wachezaji kadhaa muhimu, akiwemo Bruno Fernandes aliyesimamishwa na Lisandro Martinez na Raphael Varane ambao ni majeruhi, lakini Ten Hag alisisitiza kwamba, hawakuwa na kisingizio.

"Lazima tufanye vizuri zaidi, hilo ndilo hitaji," alisema akiiambia BT Sport.

"Tulipoteza vita, walikuwa na shauku zaidi, nia zaidi, utayari zaidi. Hiyo ni ngumu kushinda michezo.

"Inahusu wachezaji waliopo uwanjani. Wanatakiwa kufanya vizuri, ninawaamini na kuwaamini, lakini ni lazima waoneshe kiwango na hawakuwa wazuri vya kutosha.

"Tumeonyesha mara nyingi mambo mazuri, lakini usiku wa leo (juzi) hatukuwa tayari kwa mchezo. Kwa kiwango hiki, kucheza kwa Manchester United, lazima uwe tayari kwa kila mchezo.

"Hii ilikuwa fursa nzuri, hafla nzuri, kushinda kitu, na tuliiacha - lazima tujilaumu.

"Imepita, hatuwezi kuibadilisha. Tunapaswa kutazamia Jumapili (dhidi ya Brighton and Hove Albion katika nusu fainali ya Kombe la FA), hiyo ndiyo fursa inayofuata."

Christian Eriksen pia alikubali United hawakuwa kwenye mbio hizo huku wakipoteza fursa ya kurejea nusu fainali kwa mara ya tatu katika misimu minne.

"Mambo mengi yalitokea. Hatukuwapa mchezo kutoka dakika ya kwanza, na tuliwapa nafasi nyingi za kumaliza," alisema kiungo huyo.

"Ukitoa mabao kama tulivyofanya, unapoteza, mchezo wetu wenyewe haukuwa na nguvu ya kutosha, ni mpira wa miguu, wakati mwingine una siku nzuri, wakati mwingine una siku mbaya, na ilikuwa siku mbaya.

"Kila mchezaji wa soka hufanya makosa, walituadhibu mara moja. Ni jinsi tunavyorudi nyuma, na leo (juzi) hatukuwa na nguvu ya kutosha kurejea kutokana na makosa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,104,5
MECHI KALI
MANCHESTER CITY
VERSUS
SHEFFIELD UTD
1 | 1.16
X | 6.61
2 | 12.17
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MOURINHO AMPIGIA SALUTI DYBALA



**ROME,** Italia

JOSE Mourinho amempigia saluti Paulo Dybala baada ya bao lake la dakika za mwisho la kusawazisha kutayarisha njia ya ushindi mnono kwenye muda wa ziada wa AS Roma dhidi ya Feyenoord katika robo fainali ya Ligi ya Europa, Alhamisi.

Giallorossi hao walitinga nusu fainali na Bayer Leverkusen baada ya kutoka nyuma na kuishinda Feyenoord kwa jumla ya mabao 4-2 kwenye uwanja wa Olimpico.

Wakiwa nyuma kwa bao 1-0 katika mechi ya kwanza, Roma walikuwa kwenye ukingo wa kuondolewa baada ya bao la kichwa la Igor Paixao kusawazisha lile la awali la Leonardo Spinazzola.

Lakini Dybala, ambaye alianzishwa kama mchezaji wa akiba baada ya kukosa kwenye ushindi wa Jumapili dhidi ya Udinese kutokana na jeraha, alifunga bao la pili kwa Roma kwenye dakika za majeruhi na kufanya mchezo huo kwenda muda wa ziada, ambapo mabao zaidi kutoka kwa Stephan El Shaarawy na Lorenzo Pellegrini yaliwapeleka nusu fainali.

Lilikuwa ni bao la 16 la fowadi huyo wa zamani wa Juventus msimu huu na la nne katika Ligi ya Europa na uchezaji wake ulipata sifa kutoka kwa kocha wake.

"Hisia zangu ni kwamba alikuwa akitafuta furaha, alikuwa amepoteza zaidi kujiamini," alisema Mourinho akiiambia Sky Sport Italia.

"Ameipata hapa amepata kocha anayemuelewa, umati wa watu wanaompenda na nafasi uwanjani kuwa kiongozi mwenye ubora na haiba yake.

"Dybala ni kijana mzuri. Ana ubora wa kuchezea klabu kubwa duniani, lakini amepata furaha hapa.

"Nilimpa uhuru kamili wa kuingia usiku wa leo (juzi), na angeweza kutoka hata dakika mbili baadaye kama angekuwa hajisikii. Lakini alicheza dakika 30 za muda wa ziada na dakika 25 za kawaida, na akamaliza kwa kasi."

Dybala pia alitoa pongezi kwa Mourinho ambaye, baada ya kuiongoza Roma kutwaa taji la Ligi ya Europa Conference msimu uliopita, anakaribia kubeba taji la sita katika mashindano ya Ulaya.

"Nadhani kila mtu anamjua Mourinho, historia yake, alichofanya Ulaya na katika kila klabu aliyofanya kazi, nadhani alishinda kitu," fowadi huyo aliongeza.

"Akili yake inakuchangamsha. Alijua mchezo unaweza kuisha hivi na akatusukuma kutoa kila kitu zaidi. Alibadilisha mfumo wa kimbinu, tukaanza kucheza vizuri na kutawala muda wa ziada kwa ushindi unaostahili.

"Nadhani sote tunataka kushinda, ambalo ndilo jambo muhimu zaidi. Tuna kocha mwenye mawazo ya ajabu. Alituambia mchezo utakuwa hivyo, na alikuwa sahihi kabisa.

"Kikosi hiki kilishinda Ligi ya Europa Conference msimu uliopita, kwa hiyo wanajua nini kinahitajika ili kushinda. Sasa, tunatumanii kwenda kwenye Ligi ya Europa pia."



# Gundogan akanusha kumalizana na Barca

**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa Manchester City, Ilkay Gundogan amekanusha madai kwamba amefikia makubaliano binafsi na Barcelona.

Mkataba wa Gundogan unamalizima mwishoni mwa msimu huu na imeripotiwa kwamba atajiunga na vinara hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barca kama mchezaji huru.

Lakini kiungo huyo wa kimataifa wa Ujerumani amesema kwamba, hajamua bado wapi atacheza msimu wa 2023-24.

Alisema: "Majaliwa yangu hayajaamuliwa bado. Kwa uhakika kuna mazungumzo yanaendelea. Lakini siwezi kutoa taarifa zaidi kwa sasa.

"Nina furaha hapa Manchester City na napambana kushinda mataji. Pia nina furaha kuwa nahodha wa timu hii."

Aliongeza: "Unatakiwa kusubiri kujua kuhusu majaliwa yangu ya baadae."

Gundogan ameshinda mataji manne ya Ligi Kuu tangu alipojiunga na City akitokea Borussia Dortmund mwaka 2016, pia amenyakua mara nnne taji la EFL na FA mwaka 2019.

Alikiongoza kikosi cha Pep Guardiola kwenye sare ya 1-1 na Bayern Munich Jumatano, na kuwafanya wapate ushindi wa uwiyano wa mabao 4-1 na kutinga nusu fainali ya Ligi ya mabingwa Ulaya na watacheza dhidi ya Real Madrid.

City inasaka mataji matatu msimu huu, ligi ya mabingwa Ulaya, Ligi Kuu na FA.

80,144/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 22/04/23 | 17:00 | Brentford FC vs Aston Villa | 2.41 | 3.20 | 2.75 |
| 02. 22/04/23 | 17:00 | Leicester City vs Wolverhampton Wanderers | 2.38 | 3.15 | 2.85 |
| 03. 22/04/23 | 19:30 | Preston North End vs Blackburn Rovers | 2.46 | 3.20 | 2.70 |
| 04. 22/04/23 | 21:00 | FC Groningen vs NEC Nijmegen | 2.75 | 3.15 | 2.44 |
| 05. 22/04/23 | 21:45 | Sampdoria Genoa vs Spezia Calcio | 2.46 | 3.10 | 2.75 |
| 06. 23/04/23 | 10:00 | Kawasaki Frontale vs Urawa Red Diamonds | 2.37 | 3.10 | 2.55 |
| 07. 23/04/23 | 13:30 | Kasimpasa Istanbul vs Konyaspor | 2.47 | 3.25 | 2.35 |
| 08. 23/04/23 | 15:30 | PSV Eindhoven vs Ajax Amsterdam | 2.32 | 3.40 | 2.75 |
| 09. 23/04/23 | 16:00 | AFC Bournemouth vs West Ham United | 2.85 | 3.15 | 2.39 |
| 10. 23/04/23 | 16:00 | AC Ajaccio vs Stade Brest 29 | 2.95 | 3.00 | 2.42 |
| 11. 23/04/23 | 18:05 | Montpellier HSC vs Stade Rennes | 2.95 | 3.30 | 2.24 |
| 12. 23/04/23 | 18:30 | Brighton & Hove Albion vs Manchester United | 2.32 | 3.45 | 2.70 |
| 13. 23/04/23 | 18:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.55 | 3.40 | 2.49 |
| 14. 23/04/23 | 20:30 | Borussia Monchengladbach vs Union Berlin | 2.28 | 3.20 | 2.95 |
| 15. 23/04/23 | 21:45 | Juventus Turin vs SSC Napoli | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 16. 23/04/23 | 21:45 | Olympique Lyon vs Olympique Marseille | 2.37 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 23/04/23 | 22:00 | Sevilla FC vs Villarreal CF | 2.85 | 3.25 | 2.34 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 22/04/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 4137 | Fulham vs Leeds | 2.28 | 3.28 | 2.89 |
| 15:00 | 5522 | Osasuna vs Betis | 2.50 | 3.00 | 2.80 |
| 16:00 | 1504 | St Etienne vs Metz | 2.19 | 3.21 | 3.11 |
| 16:00 | 2715 | Salernitana vs Sassuolo | 2.99 | 3.34 | 2.19 |
| 16:00 | 3553 | Ruvu Shooting vs Azam | 3.43 | 2.71 | 1.77 |
| 16:00 | 3840 | Green Buffaloes vs Zesco United | 3.14 | 2.78 | 2.32 |
| 16:00 | 3969 | Zanaco vs Kansanshi Dynamos | 2.17 | 2.72 | 3.55 |
| 16:30 | 3581 | Hertha BSC vs Werder Bremen | 2.21 | 3.35 | 2.95 |
| 16:30 | 4021 | Mainz vs Bayern Munchen | 4.66 | 4.09 | 1.59 |
| 16:30 | 5729 | Hoffenheim vs FC Koln | 2.15 | 3.35 | 3.05 |
| 16:30 | 5857 | VfL Bochum vs VfL Wolfsburg | 2.90 | 3.35 | 2.24 |
| 17:00 | 1071 | Wigan vs Millwall | 3.55 | 3.30 | 1.98 |
| 17:00 | 1871 | Sheffield Wed vs Exeter | 1.37 | 4.54 | 7.66 |
| 17:00 | 1903 | Leicester vs Wolverhampton | 2.36 | 3.16 | 2.86 |
| 17:00 | 1938 | Cheltenham vs Forest Green | 1.75 | 3.54 | 4.44 |
| 17:00 | 1975 | Hull City vs Watford | 2.50 | 3.20 | 2.65 |
| 17:00 | 2147 | Dynamo Kiev vs Shakhtar Donetsk | 3.29 | 3.29 | 1.99 |
| 17:00 | 2488 | Cardiff vs Stoke City | 2.37 | 3.15 | 2.85 |
| 17:00 | 2655 | Coventry vs Reading | 1.57 | 3.66 | 5.62 |
| 17:00 | 2872 | Burnley vs QPR | 1.35 | 4.69 | 7.39 |
| 17:00 | 3233 | Celtic vs Motherwell | 1.09 | 8.81 | 18.03 |
| 17:00 | 3358 | Brentford vs Aston Villa | 2.42 | 3.19 | 2.74 |
| 17:00 | 3483 | Derby vs Burton | 1.45 | 4.35 | 6.28 |
| 17:00 | 3528 | Barnsley vs Oxford Utd | 1.73 | 3.63 | 4.44 |
| 17:00 | 4002 | Liverpool vs Nottingham | 1.20 | 5.89 | 11.59 |
| 17:00 | 4018 | Bristol City vs Rotherham | 1.99 | 3.46 | 3.36 |
| 17:00 | 4863 | Norwich City vs Swansea | 2.05 | 3.35 | 3.30 |
| 17:00 | 5644 | Birmingham vs Blackpool | 2.07 | 3.24 | 3.34 |
| 17:15 | 3754 | FC Cartagena vs Sporting Gijon | 2.07 | 3.10 | 3.50 |
| 17:15 | 4383 | Palermo vs Benevento | 1.98 | 3.20 | 3.67 |
| 17:15 | 5452 | Almeria vs Athletic Bilbao | 3.85 | 3.55 | 1.82 |
| 17:30 | 2005 | Famalicao vs Maritimo | 1.87 | 3.36 | 3.97 |
| 17:30 | 4302 | Sporting Farense vs Penafiel | 1.98 | 3.18 | 3.64 |
| 18:00 | 5112 | AJ Auxerre vs Lille | 4.41 | 3.76 | 1.67 |
| 18:45 | 1866 | Manchester City vs Sheffield Utd | 1.16 | 6.61 | 12.17 |
| 19:00 | 1905 | Lazio vs Torino | 1.81 | 3.24 | 4.39 |
| 19:00 | 3380 | Dodoma FC vs KMC | 2.25 | 2.80 | 3.24 |
| 19:00 | 5936 | Umraniyespor vs Besiktas | 4.21 | 3.73 | 1.73 |
| 19:00 | 5956 | Zenit St Petersburg vs Dinamo Moscow | 1.47 | 4.30 | 5.66 |
| 19:30 | 1103 | Valladolid vs Girona | 2.39 | 3.31 | 2.71 |
| 19:30 | 2757 | Borussia Dortmund vs Eintracht Frankfurt | 1.58 | 4.19 | 4.59 |
| 19:30 | 3157 | Real Sociedad vs Rayo Vallecano | 1.63 | 3.50 | 5.21 |
| 19:30 | 4470 | Las Palmas UD vs Levante | 2.33 | 2.95 | 3.10 |
| 19:30 | 5977 | Preston vs Blackburn | 2.50 | 3.06 | 2.76 |
| 20:00 | 5712 | Boavista vs Rio Ave | 2.29 | 3.11 | 3.06 |
| 20:00 | 5965 | Maccabi Netanya vs Maccabi Tel Aviv | 4.53 | 3.60 | 1.64 |
| 21:45 | 3296 | Sampdoria vs Spezia | 2.44 | 3.10 | 2.80 |
| 22:00 | 3744 | Real Madrid vs Celta Vigo | 1.41 | 4.48 | 6.35 |
| 22:00 | 4776 | Lens vs Monaco | 2.07 | 3.45 | 3.15 |
| 22:30 | 5040 | Pacos Ferreira vs Porto | 8.83 | 5.02 | 1.29 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MZIZE KAPANIA KWELI KWELI

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa Klabu ya Yanga, Clement Mzize amesema atapambana kuipa ushindi timu yake katika mchezo wa kesho wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Rivers United ya Nigeria.

Akizungumza na Nipashe Mzize alisema anafahamu mchezo huo utakuwa na ushindani mkali hivyo amejipanga kutumia nguvu na akili nyingi akishirikiana na wachezaji wenzake.

**"Dabi ya Yanga na Simba imemalizika ingawa hatuku pata matokeo mazuri, lakini sasa hivi naelekeza nguvu na akili zangu kwenye mch ezo wetu wa Robo fainali," alisema Mzize.**

Alisema atatumia maelekezo aliyopewa na benchi lake la ufundi ambayo anaamini yatampa mafanikio.

Aidha alisema anataka kujituma zaidi kwenye kikosi cha Yanga ili aweze kitimiza malengo yake ya kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi.

"Malengo yangu ni kucheza soka la kulipwa nje ya nchi, lakini lazima kwanza niimarishe kiwango changu hapa Yanga," alisema.

Aliwaahidi mashabiki wake kuendeleza kiwango chake ili aweze kupata namba kwenye kikosi hicho.




# Tutawakanda tu

INATOKA UK 24

naimarisha safu ya ulinzi kutokana na ubora wa wapinzani wao watatumia vizuri nafasi wanazotengeneza kutafuta mabao na kufikia malengo yao ya kusonga mbele.

Rais wa heshima na muwekezaji wa Simba, Mo Dewji alisema mwaka 2003 walivyokuwa wanacheza na Zamalek ya Misri ambao walikuwa mabingwa watetezi wa ligi ya Mabingwa Afrika hakuna aliyetegemea.

Alisema ana imani kubwa na timu hiyo kufikia rekodi hiyo kwa sababu ya kuwepo kwa imara wa kikosini chao huku wachezaji wamemhakikishia kupata matokeo mazuri.

Mo Dewji alisema kipindi kile Zamalek ilikuwa inatisha na kila timu inayokutana nayo hasa kutoka kwenye ukanda wa Afrika Mashariki ilikuwa ikipata kipigo.

"Nimekaa na Mtendaji Mkuu (Imani Kajula), Mwenyekiti wa Bodi, Salim Abdallah (Try Again) na wachezaji kuwaandaa kisaikolojia kwa ajili ya mechi hii.

"Hadithi ya kila siku Simba kucheza robo au kufika 10 bora ya Afrika haitoshelezi, tunahitaji sasa kusonga mbele, nina imani kubwa na wachezaji watapambana Jumamosi kupata mabao mengi zaidi," alisema Mo Dewji.

# Yanga SC: Safari hii hatuwaachi ng'o

INATOKA UK 24

yao ipo kwenye mechi hiyo, tulianza mazoezi siku mbili Dar es Salaam, huku pia tuna siku mbili za mazoezi, tunaamini tutakuwa na mpango mzuri wa kimbinu baada ya kuwasoma vizuri wapinzani wetu Rivers United," alisema Kamwe.

Timu hizo zilikutana msimu uliopita kwenye hatua ya awali Ligi ya Mabingwa, Yanga ikitolewa kwa jumla ya mabao 2-0, Septemba 12, 2021 ikifungwa bao 1-0 nyumbani na kwenda kufungwa tena bao 1-0 ugenini, Septemba 19 mwaka huo.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Aprili 22, 2023




Ten Hag akosoa uchezaji wa Man Utd UK. 21



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kujiandaa na mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Wydad Casablanca leo. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Tutawakanda tu

## Simba yapanga kuivunja rekodi iliyoweka kwa Zamalek 2003 ikiivaa Wydad leo...

**Na Saada Akida**

SIMBA imepanga kuingia kivingine katika mchezo wao wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mabingwa watetezi wa michuano hiyo, Wydad Casablanca leo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kuanzia majira ya saa 10:00 Alasiri.

**Kwenye mchezo huo Simba itakosa huduma ya Golikipa wao namba moja, Aishi Manula ambaye ni majeruhi na yuko chini ya uangalizi wa madaktari.**

Mchezo huo ni muhimu kwa viongozi wa Simba na unachukuliwa kama sura mpya na kipekee baada ya Rais wa heshima na muwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed Dewji jana jioni kukutana na wachezaji kuzungumza nao kabla ya mchezo huo.

Simba imedhamilia kufikia rekodi yao ya mwaka 2003 ya kumtoa bingwa mtetezi wa Afrika kwa wakati huo, Zamalek ambapo Wydad ni mabingwa watetezi wa sasa.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera Robertinho akizungumza jana na waandishi wa habari kuelekea mchezo huo alisema wamefanya maandalizi mazuri na wako tayari kuwakabili Wydad.

Alisema mechi itakuwa ya ushindani, lakini ameandaa kikosi chake kwa kuingia na mipango ya kushinda katika mchezo huo na wamejipanga kupata idadi kubwa ya mabao ili kujiweka kwenye nafasi nzuri zaidi katika mchezo wa marudiano.

"Tupo tayari kwa mchezo huu na nina imani tutashinda sababu wachezaji wangu wana ari kubwa ya kupambana najua utakuwa mchezo mgumu kutokana na ubora walionao wapinzani wetu, lakini tupo tayari kwa mapambano lengo ni kupata ushindi," alisema.

Aliongeza: "Tutacheza mchezo huo kwa nidhamu kubwa na heshima kwa sababu ni mabingwa watetezi, ila nina imani sana na vijana wangu kuwa watafanya kile nilichowapa mazoezi.

"Tangu siku ya kwanza ya mashindano haya niliona Simba inauwezo wa kufika mbali na hata kubeba kabisa taji lenyewe," alisema Robertinho.

Kwa upande wa Shomari Kapombe ambaye aliwawakilisha wachezaji wenzake, alisema maandalizi ni mazuri na ni wakati mzuri na sahihi kukutana na timu kubwa Afrika na kuonesha ubora wao kuwa wanauwezo wa kupambana nao.

"Benchi la ufundi limemaliza kazi, jukumu kubwa limebaki kwetu sisi wachezaji kufanya vizuri uwanja wa nyumbani kwa kutafata ushindi wa mabao mengi, tuna waheshimu Wydad kwa sababu wanataka kulinda ubingwa wao. Lakini sisi tunahitaji kutumia vizuri uwanja wa nyumbani na kufanya kile ambacho walifanya waliotangulia mwaka 2003," alisema Kapombe.

Aliongeza kuwa wanatambua mechi yao ya marudiano itakayopigwa nchini Morocco haitakuwa nyepesi, lazima wapambane kutafuta ushindi wa mabao mengi zaidi ya kwenye uwanja wa Mkapa kabla ya kurejeana Aprili 28, mwaka huu.

"Safari hii tunahitaji kutinga nusu fainali, robo hii imekuja tofauti na zile zilizopita kwa sababu ni misimu mitatu tunatolewa katika hatua hii. Safari hii tunahitaji kufanya kile walichokifanya waliotangulia kwa kumuondoka bingwa mtetezi ili tuweze kutinga nusu fainali," alisema Kapombe.

Kwa upande wa kocha Mkuu wa Wydad, Juan Carlos alisema ni mechi muhimu na Simba ni timu nzuri ina wachezaji wazuri, lakini wao malengo yao ni kuvuka hatua hii na kusonga mbele.

Alisema wanafahamu mchezo utakuwa mgumu na watafanya kila kinachowezekana ili kupata matokeo mazuri, kwa sababu wako kwenye nafasi ya kipekee wakishinda wanapata uhakika wa kusonga mbele.

"Kikubwa na muhimu ni kusonga mbele kwa kukabiliana na mpinzani wetu kwa hali yeyote, kucheza vizuri, kushambulia tukiwa na mpira na kuzuia tunapokuwa na mpira," alisema.

"Simba ni timu nzuri inapocheza nyumbani na wamejiandaa vizuri kwa asilimia 100 kwa kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu ili kufanikiwa malengo ya kuondoka na matokeo mazuri," aliongeza.

Alisema kutambua mechi ya leo wa-

INAENDELEA UK 23

## Yanga SC: Safari hii hatuwaachi ng'o

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze amesema watahakikisha makosa yote yaliyojitokeza kwenye mechi dhidi yao na watani zao wa jadi Simba hayajirudii tena nchini Nigeria hapo kesho itakapocheza dhidi ya Rivers United.

AkIzungumza akiwa nchini humo kuelekea mechi ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika itakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Godswill Akpabio nchini humo karika mji wa Akwa majira ya saa 10:00 jioni kwa saa za Afrika Mashariki, Kaze alisema wamekuwa wakiyafanyia kazi makosa yote yaliyoonekana kwenye mechi ya Jumapili iliyopita ambapo walifungwa mabao 2-0 na Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, hasa upande wa mabeki na mipira ya kutenga.

"Tuliona makosa tuliyoyafanya kwenye 'dabi' na hasa upande wa mabeki na pia hata kwenye mipira ya kutenga, ila tunaamini kuwa huu ni mchezo tofauti na una mbinu tofauti, tumeiangalia vizuri timu tunayokwenda kucheza nayo, naamini tutafanya vizuri, alisema Kaze.

Kuhusu makosa ya mara ya kwa mara ya mabeki wake kuruhusu mabao ya faulo, alisema wamekuwa wakiwaelekeza wachezaji jinsi ya kufanya, lakini pamoja na yote hayo, kitendo cha mchezaji kuruka juu na kuufuata mpira kuupiga kichwa kinabaki kuwa ni tabia ya mchezaji mwenyewe.

"Ni kweli tumekuwa tukifungwa huko nyuma, tukalifanyia kazi, na kama utaona ikapita mechi saba au nane hatukuruhusu bao la aina hiyo mpaka Jumapili iliyopita dhidi ya Simba, kwa hiyo utaona hata kama ukifundisha lakini hiyo ni tabia ya mtu au mchezaji mwenyewe tangu alipoanza kucheza soka kupenda kuzuia mpira ya faulo kwa kuwahi kuruka kichwa, au kutomuachia mtu ambaye anamkaba," alisema Kaze.

Kwa upande wa Ofisa habari wa Yanga, Ally Kamwe alisema kikosi kimefika salama na wachezaji wao wameweka vizuri kisaikolojia hasa baada ya kupoteza mechi ya 'dabi' dhidi ya Simba.

"Hali ya kikosi kiko salama kabisa, mambo yanakwenda vizuri sana. Huu ni mchezo wa robo fainali ambao una mechi mbili, ni hatua kubwa, ukishafika hapa ujue unakwenda kucheza na timu nzuri. Tumepoteza mchezo wa'dabi' ni lazima tuwaweke vizuri kwanza wachezaji wetu kisaikolojia, ninapozungumza na wewe wachezaji wote akili

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >